# Nipashe

Jumatatu Machi 18, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579868

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper




## DC, vigogo wanne waingia mikononi mwa Takukuru

UKURASA 12




UKURASA 13

# Serikali yatangaza siku 15 malipo wakulima korosho

UKURASA 3



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akionyesha nakala za kitabu cha I can, I must, I will zilizoandikwa kwa mfumo wa nukta nundu ili kuwawezesha watu wasioona kukisoma baada ya kukizindua jana, jijini Dar es Salaam. Kitabu hicho kimetungwa na Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi (kushoto). Wengine ni Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier (wa pili kulia) na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe (wa tatu kulia). **PICHA: HALIMA KAMBI**

## Mfuko asasi zinazosaidia watu wenye ulemavu kuanzishwa

UKURASA 2

## Onyo kali Ma-DED wala fedha za miradi

UKURASA 5

**MICHEZO** SIMBA ILIVYOITEKA AFRIKA KIPIGO AS VITA UK. 18

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Serikali yajipa wiki 2 malipo ya korosho

**Na Mathias Canal,** LINDI

SERIKALI imeihakikishia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuwa kufikia mwisho wa mwezi huu, wakulima wote wa korosho watakuwa wamelipwa fedha zao baada ya uhakiki kukamilika kwa kiasi kikubwa.

Hakikisho hilo lilitolewa juzi na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alipotoa ufafanuzi katika mkutano uliowakutanisha wajumbe wa kamati hiyo, viongozi wa serikali, wataalamu na wakulima mkoani Lindi.

"Kumekuwa na urasimu mkubwa tangu kuanza kwa uhakiki, lakini sasa tumeamua kama serikali kabla ya mwisho wa mwezi huu wa tatu (mwezi huu), wakulima wote wawe wamelipwa malipo yao ili kuondoa adha wanazokumbana nazo," Hasunga alisema.

Waziri huyo alisema mchakato wa malipo unahitaji kupitia katika hatua nyingi ikiwamo uhakiki, lakini kila jambo lenye mwanzo ni lazima kuwa na ukomo.

Alibainisha kuwa mpaka sasa, tani 222,684 za korosho zimekusanywa na hadi kufikia Ijumaa iliyopita, Sh. bilioni 596.9 zilikuwa zimeshalipwa kwa wakulima kati ya Sh. bilioni 723 wanazodai.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Christine Ishengoma, alimwagiza waziri huyo kuhakikisha taarifa ya malipo ya wakulima wote wa korosho inafika bungeni Aprili 2, mwaka huu.

Hasunga pia alisema wizara imepitia hatua mbalimbali ya kumpata Mkurugenzi mpya wa Bodi ya Korosho ili kuendelea na majukumu ya bodi hiyo.

Alisema hatua mbalimbali pia zimeanza kuchukuliwa dhidi ya wafanyabiashara wote waliofanya hujuma kwa kuwauzia wakulima mbegu na mbolea feki.

Waziri huyo aliuagiza uongozi wa Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu vya Tropiki (TPRI) kutuma wataalamu mkoani Lindi kuchukua sampuli za viuatilifu kwa wakulima na kuzipima ili kujua ukweli wa madai ya kuwapo kwa viuatilifu feki vilivyosambazwa kwa wakulima.



Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, akizungumza na wananchi na wanafunzi katika viwanja vya Shule ya Msingi Meru mkoani humo, katika matembezi ya uhamasishaji wa umma kuhusu umuhimu wa afya ya kinywa na meno, ambapo kilele chake kitakuwa keshokutwa. **PICHA: HAMISI MUSA**

# Apongeza shirika kuokoa mabilioni

**Na Munir Shemweta,** MISENYI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, amelipongeza Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), kwa kuokoa mabilioni ya shilingi yaliyokuwa yatumike kujenga Kitega Uchumi cha Mtukula kilichoko Misenyi mkoani Kagera.

Mabula alitembelea mradi wa ujenzi wa jengo hilo wakati akiwa kwenye ziara ya kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia sekta ya ardhi katika Wilaya ya Misenyi mwishoni mwa wiki.

Alieleza kufurahishwa na gharama ndogo zilizotumika katika ujenzi wa kitega uchumi hicho cha NHC Mtukula baada ya kuelezwa na Mhandisi wa Ujenzi, George Shanel, kuwa hadi sasa, gharama yake imefikia Sh. milioni 800 wakati jengo limefikia asilimia 80 ya ujenzi.

Kiwango hicho ni tofauti na makadirio yaliyoelezwa awali kuwa lingegharimu Sh. bilioni tatu kama ujenzi huo ungefanywa na kampuni ambayo ingepewa zabuni.

Mabula alilipongeza shirika kwa kuokoa fedha nyingi kwa kutumia kampuni yake ya ujenzi na kutoa wito kwa taasisi mbalimbali nchini kulitumia shirika hilo kujenga ofisi na nyumba za watumishi kwa kuwa lina uwezo mkubwa katika ujenzi.

Jengo la kitega uchumi la NHC Mtukula liko mpakani mwa Tanzania na Uganda, litakapokamilika, litakuwa na ofisi mbalimbali zikiwamo za benki na maduka 36.

Mabula alisema kufanya vizuri kwa shirika hilo kumejionyesha katika kazi za ujenzi wa ofisi za wizara mbalimbali katika Mji wa Serikali Ihumwa mkoani Dodoma, linakojenga ofisi za wizara mbalimbali zikiwamo Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Fedha na Mipango.

Alidai ujenzi unaotekelezwa na shirika hilo Ihumwa unakwenda kwa haraka na ubora wa uhakika.

# Auawa na polisi akidaiwa jambazi

**Na Steven William,** MUHEZA

JESHI la Polisi wilayani Muheza mkoani Tanga limemuua kwa kumpiga risasi Mkazi wa Dar es Salaam, Mwinyiheri Nuhu, likidai alikuwa anajihusisha na ujambazi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, alidai jana kuwa Nuhu alikuwa miongoni mwa watuhumiwa wanne wa ujambazi waliovamia nyumba ya mfanyabiashara Ally Nassoro wilayani Muheza wakiwa na bunduki juzi usiku.

Alisema tukio la kuuawa kwa mtuhumiwa huyo wa ujambazi lilitokea juzi usiku saa nne usiku katika Kijiji cha Songa wilayani humo ambako mfanyabiashara huyo anaishi.

Kamanda Bukombe alidai watuhumiwa hao wa ujambazi walivamia nyumbani kwa mfanyabiashara huyo wakitumia gari ndogo na kupora Sh. milioni moja zilizokuwako.

Alidai kuwa wakati watuhumiwa hao wakiendelea kufanya uhalifu, askari polisi kutoka vituo vya Wilaya ya Muheza na Hale wilayani Korogwe, walifika kwenye nyumba hiyo na kuanza kupambana nao kwa kurushiana risasi.

Kamanda Bukombe alidai kuwa wakati wakirushiana risasi, polisi walimuua Nuhu, lakini wenzake walitoroka na wanaendelea kusakwa na jeshi hilo.

Alidai walinasa bunduki mbili, kitambulisho cha Nuhu na Sh. milioni moja zilizokuwa zimeporwa kutoka kwa mfanyabiashara huyo.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 16/03/2019.

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe **20/03/2019** kampuni ya **S.S.F Co.LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea KAGERA SUGAR** gari hilo lenye namba za usajili:

**T776 CAD/T 243DCT.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

Urefu - mita 18
Upana - mita 3.0
Kimo - mita 5.2

3. NJia itakayotumika DAR hadi **KAGERA kupitia MWENDAKULIMA** gari litasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

21512102



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 16/03/2019.

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumatano tarehe 20/03/2019** kampuni ya **S.S.F Co.LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea KAGERA SUGAR** gari hilo lenye namba za usajili:
**T794 DFQ/T 394 ADH.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**Urefu - mita 19**
**Upana - mita 3.2**
**Kimo - mita 5.2**

3. NJia itakayotumika **DAR hadi KAGERA kupitia MWENDAKULIMA** gari litasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

21512102

## Harakati ukombozi Afrika kuhifadhiwa

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

SERIKALI imesema itakarabati maeneo yote ya kihistoria yaliyotumika katika harakati mbalimbali za ukombozi wa Afrika ili kutunza na kuhifadhi kumbukumbu zake.

Kauli hiyo ilitolewa jana wilayani Kaliua mkoani Tabora na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, wakati wa ziara ya kutembelea maeneo ya urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika likiwamo eneo lenye historia ya makazi ya Shujaa wa Afrika Mashariki na Kati, Mtemi Mirambo.

Waziri huyo alisema lengo la ukarabati huo ambao serikali inaendelea kuutafutia fedha, ni kutunza historia ya mashujaa na maeneo waliyoyatumia na kuwafanya vijana wa sasa na vizazi vijavyo waujue ukweli wa historia za mashujaa wote wa taifa pamoja na wapigania uhuru wa Afrika.

Alisema ukarabati huo unakwenda sambamba na kutafuta kumbukumbu zote walizotumia wapigania uhuru mbalimbali ili kuzitambua na kuzihifadhi rasmi kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo na kuendeleza ulinzi wa kazi hizo za kihistoria.

Waziri Mwakyembe alitoa wito kwa Watanzania wote wenye taarifa za kumbukumbu mbalimbali zikiwamo picha, vitabu, mashairi, nyimbo, barua na nyaraka mbalimbali zilizotumiwa na wapigania uhuru wa Tanzania na nje ya nchi, kuziwasilisha Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo au kwa viongozi wa serikali za mitaa ili zitunzwe kwa ajili ya manufaa ya taifa na Afrika.

Aliwataka wananchi na viongozi wa serikali za mitaa kulinda alama zote zilizoko katika maeneo yaliyotumiwa na wapigania uhuru ikiwamo majina katika makaburi na majengo ili kutopoteza kumbukumbu za mashujaa.

Katika hatua nyingine, Waziri Mwakyembe aliwataka wataalamu mbalimbali na maofisa utamaduni nchini, kutumia hazina ya wazee walioko katika maeneo yao wanaojua historia ya kweli kuhusu harakati za kudai uhuru nchini na mapambano ya ukombozi barani Afrika, kupata maelezo na kuyaandika kwa ajili ya kuweka kumbukumbu zake.

"Tunajua kila mtu atakufa, hivyo ni vema tukatumia hazina ya wazee wetu waliopo sasa kupata historia ya kudai uhuru na harakati za ukombozi zilizofanyika nchini ili kuweka kumbukumbu zote zikiwamo picha na maneno yao," waziri huyo aliagiza.

Alisisitiza kuwa simulizi ya wazee ni muhimu katika kuhakikisha hakuna mashujaa walioshiriki harakati za kudai uhuru na ukombozi wa Bara la Afrika zitakazoachwa katika kuandika na kuweka taarifa za kazi zao kihistoria.

### KUVULIWA UBUNGE:

## Nassari ajitetea, aamua kukimbilia mahakamani

**Na Enock Charles**

SIKU chache baada ya Spika Job Ngugai kutangaza kumvua ubunge Joshua Nassari, kwa madai ya kupoteza sifa za kuwa mbunge kutokana na utoro, mwanachama huyo wa Chadema amejitetea na kueleza dhamira yake ya kulipeleka mahakamani suala hilo.

Spika Ndugai alitangaza Alhamisi kumvua Joshua ubunge wa Arumeru Mashariki kwa madai ya kutohudhuria mikutano mitatu mfululizo ya Bunge, kinyume cha Kanuni za Bunge na Katiba ya nchi.

"Naomba niwahakikishie watu wa Meru kwamba haki yao ya uwakilishi ndani ya Bunge na maelfu ya wananchi waliojipanga kupiga kura ili kuwa mwakilishi wao, tutaipigania mahali popote na kwa kuanzia, tutakwenda kwenye vyombo vya sheria mahakamani, Nassari alisema katika mkutano wake na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana. Alidai Ofisi ya Spika imefanya uamuzi wa kumvua ubunge bila kumsikiliza na kusisitiza kuwa alitoa taarifa kwa barua pepe kuhusu kuuguliwa na mkewe aliyekuwa amejifungua Marekani.

"Ni kwa muda sasa, mimi na mke wangu tumekuwa na matatizo ya kiafya," Nassari alisema, "sina haja ya kuongelea kwa undani kwa kuwa ni masuala ambayo ni siri kati ya daktari na mgonjwa." Akieleza zaidi kuhusu sababu zlizomfanya kushindwa kuhudhuria bungeni katika mikutano mitatu mfululizo kama ilivyodaiwa na Spika, Nassari alidai mikutano ya Novemba na Januari hakuhudhuria, huku akikanusha madai ya kutoshiriki mkutano wa Bunge wa Septemba mwaka jana.

Alidai Septemba alishiriki shughuli za Bunge na kulipwa posho na stahiki zote na ubunge na kwamba muda ukifika, ataweka kila kitu hadharani zikiwamo nakala za malipo ya benki aliyolipwa na chombo hicho cha kutunga sheria.

"Naamini hii si sahihi hata kidogo. Muda utakapofika huko mbele, tutaweka nyaraka hadharani kwa sababu kwa mfano, kwa Septemba na kamati yake nimeshiriki na kulipwa posho na stahiki ambazo wabunge wote wamelipwa na nyaraka za benki zipo, tutaweka hadharani," Nassari alidai.

Nassari alimwomba Spika Ndugai kurejea uamuzi wake kwa kuwa bado anayo nafasi ya kufanya hivyo, huku akikumbushia tukio la miaka mitano iliyopita la spika huyo kuhudhuria harusi yake wakati huo akiwa naibu spika.

"Najiuliza hivi kweli alikuja kwenye harusi na akazungumza kama mzazi ili siku moja nimwache mwenzangu ateseke peke yake kama mjane wakati nipo hai?" Nassari alihoji.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (katikati) na Meneja wa QNET Kanda ya Kusini mwa Afrika, Biram Fall (kushoto), wakikata utepe kuzindua rasmi maonyesho ya bidhaa za QNET 2019 katika ukumbi wa Mlimani City jijini humo juzi. Kulia ni Mshauri wa Biashara wa QNET Tanzania, Edward Mkony. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Sheria ya Uvuvi kufumuliwa

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imelazimika kufanya marekebisho ya dharura kwa baadhi ya vipengele vya Sheria ya Uvuvi kutokana na wananchi kushindwa kuvumilia kusubiri kukamilika marekebisho hayo Julai mwaka huu. Akizungumza jijini Mwanza jana, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, aliwaarifu wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu mpango huo wa serikali walipotembelea viwanda na kuzungumza na baadhi ya wadau wa uvuvi Kanda ya Ziwa.

Wadau waliozungumza na wajumbe wa kamati hiyo ni pamoja na wenye viwanda vya kuchakata samaki, mawakala, wafanyabiashara wa samaki na wauzaji mabondo na zana za uvuvi.

Mpina alisema serikali inafanyia marekebisho Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 kwa dharura kwa baadhi ya vipengele na kufikia Aprili 15, marekebisho hayo yatakuwa yamekamilika.

Mpina aliwaambia wajumbe kuwa vipengele viwili ndivyo vitakavyofanyia marekebisho kikiwamo cha utumiaji wa nyavu za milimita nane kwa uvuaji wa dagaa mchele baharini kwa kuwa awali sheria ilikuwa inataka milimita 10, lakini wakawa wanavulia dagaa papa ambao ni wakubwa. Alisema kutokana na changamoto hiyo, watafanya utafiti ndani ya wiki mbili na ikigundulika kweli milimita nane ndiyo inafaa, watawaruhusu wananchi wavue kwa kutumia nyavu zenye ukubwa huo.

Alisema pia yakifanyika marekebisho kipengele cha upande wa sangara kuangalia kama wana uwezo wa kurekebisha kutoka nyavu zenye ukubwa wa inchi sita hadi saba au nane kwa kuwa inaonekana nyavu zenye matundu ya inchi sita zinavua kwa wingi samaki wa sentimita 50, 75 na 85 kwa kiasi kidogo.

"Katibu Dk. Rashid Tamatamah, ameshapatiwa maagizo na ndani ya wiki mbili, kazi hiyo itakuwa imekamilika," Mpina alisema.

"Baada ya kukumbana na changamoto za wavuvi na kuona hawawezi kuvumilia mpaka ifikapo Julai Mosi, muda wa kukamilika marekebisho ya sheria, tumeona tufanye marekebisho ya dharura kwa baadhi ya vipengele ili ifikapo Aprili 15, viwe vimekamilika kwa upande wa nyavu za sangara iwe inchi saba au nane na dagaa mchele milimita nane," Mpina alisema. Akitolea ufafanuzi suala la utumiaji wa nyavu tofauti kati Dar es Salaam na Mwanza, Mpina alisema uvuvi ni sayansi, hivyo uvuvi wa bahari hauwezi kuwa sawa na wa Ziwa Victoria wala Tanganyika.

Alisema sheria ni moja lakini kanuni ni tofauti kutokana na mazingira kuwa tofauti kwa kuwa ukubwa wa sangara huwezi kuulinganisha na ukubwa wa samaki wanaopatikana baharini na pia dagaa wanaopatikana Ziwa Tanganyika huwezi kulinganisha na wanaopatikana Ziwa Victoria, hivyo hata zana zinazotumika ni tofauti. Mjumbe wa kamati hiyo, Pascal Haonga, alisema serikali inapaswa kuonyesha namna ya kutatua tatizo na kamati kazi yao itaendelea kuisimamia na kuishauri.

Katibu Mtendaji wa Muungano wa Viwanda vya Uchakataji wa Samaki (TIFPA), Onesmo Sulle, aliomba serikali kuhakikisha kunakuwa na uwiano wa utekelezaji wa Sheria ya Uvuvi katika nchi zote za Afrika Mashariki.

## HABARI KITAIFA



Mtemi Mirambo wa II, Salumoni Kazikwa (aliyechuchumaa) akimwombea Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe (aliyekaa kwenye kigoda), kwenye kaburi la shujaa wa Afrika Mashariki na Kati, Mtemi Mirambo, wakati wa ziara yake jana ya kutembelea maeneo ya urithi wa ukombozi wa bara la Afrika ikiwamo eneo la shujaa huyo. **PICHA: DAUD TIGANYA**

# Ma-DED wanaojikopesha fedha za Tasaf waonywa

**Na Abdallah Bakari,** MTWARA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa imewaonya wakurugenzi wa halmashauri, miji, manispaa na majiji wanaojikopesha fedha zinazotolewa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf).

Imesema imebaini baadhi ya wakurugenzi badala ya kzitumia fedha za mfuko huo kutekeleza miradi ya halmashauri zao, wamekuwa wakizichukua kwa ahadi kuwa wakipata pesa watazirejesha.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Jasson Rweikiza, alitoa onyo hilo mwishoni mwa wiki akiwa mkoani Mtwara walipotembelea wanufaika wa mfuko wa Tasaf III katika Kijiji cha Nemeela kilichoko Halmashauri ya Mtwara Vijijini na kuongeza kuwa kitendo hicho kinaumiza walengwa kwa kuwa hawapati fedha kwa wakati.

Alisema baadhi ya wakurugenzi wanajikopesha fedha za Tasaf kwa ahadi ya kuzirejesha watakapopata fedha nyingine, akiwataka waache mara moja mwenendo huo.

"Tabia ya wakurugenzi kubadilisha matumizi ya fedha za Tasaf kwa kuziazima, hapana, ikome! Wanarudisha lakini wakati huo wananchi wameteseka. Sisi kama kamati, tunaridhishwa na utekelezaji wa kazi za mfuko huu," alisema.

Rweikiza aliongeza: "Niwaombe wanufaika wa mradi huu wa Tasaf III mtumie fedha kwa ajili ya shughuli za kimaendeleo ili mjikwamue na hali ngumu ya kimaisha inayowakabili. Niwapongeze wale wote ambao wametumia fedha hizi kwa shughuli za kimaendeleo na kufanikiwa."

Awali, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mtwara, Dk. Jilly Maleko, alisema mkoa huo ulikuwa na wanufaika 48,950 kabla ya uhakiki kubaini wanaostahili kuendelea na mpango huo kuwaondoa 4,820, hivyo kubaki na wanufaika 44,130.

Alisema mpango wa kunusuru kaya masikini umefanikiwa kwa kiwango kikubwa mkoani Mtwara kwa kuwa wahusika wametumia fedha hizo kwa kuanzisha miradi mbalimbali ya uzalishaji mali na kuboresha makazi yao. "Wapo waliojenga nyumba bora, walioanzisha miradi ya ufugaji kuku, mbuzi na shughuli zingine za kujiongezea kipato, hali hii imeufanya mkoa ufanikiwe kikamilifu," Dk. Maleko alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, alisema serikali itaendelea kusimamia matumizi bora ya fedha za Tasaf ili kuhakikisha hakuna malalamiko yanayojitokeza katika utekelezaji ambayo yanaweza kuathiri mradi huo.

# Waziri Mkuu atoa neno utoroshaji wa madini

**Na Mwandishi Maalum**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa tahadhari kwa wadau wote wa madini kuwa atakayekamatwa anatorosha madini, atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kutaifisha madini atakayokuwa akiyatorosha.

Pia amewataka viongozi na watendaji wote wa serikali wasimamie kwa weledi, uaminifu na uadilifu, sheria, kanuni na miongozo kuhusu sekta ya madini kwa lengo la kudhibiti utoroshwaji wa madini hususan dhahabu kwenda nje ya nchi.

Waziri Mkuu alitoa tahadhari hiyo jana wakati akifungua Soko la Madini la Mkoa wa Geita. Ufunguzi wa soko hilo ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli alilotoa Januari 22, mwaka huu la kuitaka mikoa yote ianzishe masoko ya madini.

Majaliwa alizitaka Wizara ya Madini, Tume ya Madini, serikali ya mikoa, idara na taasisi nyingine za serikali zinazohusika na maendeleo ya sekta ya madini, waheshimu mipaka ya majukumu yao ili kulisimamia vizuri soko

INAENDELEA UK. 8

# DC ataka mkakati wa kuboresha shule kongwe

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKUU wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, ameuagiza uongozi wa halmashauri hiyo, kuandaa mpango mkakati utakavyoboresha na kukarabati miundombinu ya shule kongwe zilizochakaa wilayani humo.

Ndemanga alitoa agizo hilo wakati wa kupokea na kuzindua miradi miwili ya vyoo bora na vifaa kwa Shule kongwe ya Msingi Stadium iliyoko katika halmashauri hiyo.

Alisema shule kongwe kama ilivyo Stadium ni nyingi na zinahitaji kuwa na mpango mkakati maalum wa kuzikarabati ili kuzirejesha katika ubora. "Shule kongwe za aina hii zipo nyingi, majengo yake ni mabovu na hatuwezi kuyakarabati yote mara moja au kwa siku moja, hebu tuwe na mpango ambao utatuwezesha kujua tutafanya nini leo, kesho na miaka ijayo," aliagiza.

Alimtaka Mkurugenzi wa Manispaa, Jomari Satura, kwa kushirikiana na Meya wa Lindi, Mohamedi Lihumbo, kuandaa andiko linaloonyesha idadi ya majengo chakavu, kiwango cha uchakavu na gharama na hatua ambazo halmashauri itachukua ili serikali na wadau wengine wasaidie kuchangia.

Akipokea mradi huo wa vyoo vyenye matundu 24, yakiwamo mawili kwa ajili ya matumizi ya walimu, kiongozi huyo wa serikali alizishukuru Taasisi za Khaki na Lindi Islamic Foundation (LIFT) kwa kuona umuhimu wa kusaidia upatikanaji wa huduma hiyo bora kwa Shule ya Msingi Stadium.

Ndemanga alisema mtoto anapotumia choo bora, anakuwa na mawazo pale atakapokuwa na maisha yake, atajua kuwa na umuhimu wa kuwa na choo safi.

Awali, akisoma taarifa ya uzinduzi wa vyoo hivyo, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Angelina Leonard, alisema shule hiyo iliyoanzishwa Desemba 1926, ililenga kuhudumia watoto wenye asili ya Asia na ilipofika mwaka 1964, ilichukuliwa na serikali na kwamba kwa sasa ina wanafunzi 849, wasichana wakiwa 426.

Mkurugenzi wa LIFT, Hamisi Ajali, alisema ujenzi wa vyoo hivyo umegharimu Sh. milioni 43, kiwango ambacho ni chini ya bajeti iliyopangwa ya milioni 45.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Afcon inawezekana Stars ikiivaa Uganda kama fainali

**HATIMA** ya timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, kufuzu ama kutofuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon 2019) itajulikana Jumapili baada ya dakika 90 ya mtanange wa mwisho wa hatua ya makundi dhidi ya Uganda ('The Cranes') utakaopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Mechi hiyo ya Kundi L, linalojumuisha pia Cape Verde na Lesotho, ni muhimu kwa Stars kushinda ili kukata tiketi ya kushiriki fainali hizo zitakazofanyika nchini Misri Juni mwaka huu.

Katika kundi hilo Uganda iko kileleni ikiwa na pointi 13 ikifuatiwa na Taifa Stars yenye alama tano sawa na Lesotho, huku Cape Verde ikiburuza mkia kwa pointi zake nne.

Kwa Uganda itakuwa ikikamilisha tu ratiba kwa kuwa imeshafuzu kutokana na ukweli kwamba hakuna timu kwenye kundi lake inayoweza kufikisha pointi zake.

Lakini pamoja na kuwa na tiketi hiyo mkononi, bado Uganda ambayo katika mechi yake ya kwanza nyumbani ililazimishwa sare na Stars, huku michezo mingine minne ikishinda, inaonyesha kudhamiria kutopoteza mchezo wowote na leo imeingia kambini nchini Misri kujiandaa na mchezo huo.

Kwa ujumla licha ya Stars kuwa nyumbani, mechi hiyo haitakuwa rahisi kwao na kinyume cha ushindi haitaweza kufuzu fainali hizo kwa mara ya kwanza tangu 1980. Ikumbukwe kwamba Stars, Lesotho na hata Cape Verde zote zina nafasi ya kuungana na Uganda kukata tiketi ya kushiriki fainali hizo.

Hiyo ni kutokana na ukweli kwamba, endapo Stars itapoteza dhidi ya Uganda Jumapili mshindi kati ya Cape Verde na Lesotho ataungana na Uganda kufuzu fainali hizo.

Lakini pia hata kama Stars itatoka sare katika mechi hiyo ya mwisho huku timu moja kati ya Lesotho na Cape Verde ikipata ushindi iliyoshinda ndiyo itakayoungana na Uganda. Hivyo kinachotakiwa kwa Stars ili kufuzu ni kushinda tu Jumapili na si vinginevyo, jambo ambalo Nipashe tunaamini linawezekana.

Tunaamini kikosi kilichoitwa na Kocha Emmanuel Amunike, kinaweza kutimiza malengo hayo ya Tanzania kufuzu kwa mara ya kwanza baada ya miaka 30 ingawa mechi hiyo itakuwa ngumu, hilo halitupi hofu sana kwa kuwa kama Stars iliweza kupata sare ugenini dhidi ya Uganda, kupata matokeo nyumbani ni jambo linalowezekana.

Ni wazi Amunike atakuwa ametambua ni wapi kikosi chake kilifanya makosa katika mechi iliyopita na kuyafanyia kazi kabla ya Jumapili.

Lakini pia kwa siku hizi tano kabla ya Jumapili, tunaamini zinatosha kabisa kurekebisha kasoro ndogondogo za kimfumo na Stars kuweza kupata matokeo.

Nipashe tunaamini wachezaji na benchi zima la ufundi hawatatuangusha hivyo kilichobaki ni Watanzania kwa ujumla kuelekeza dua na maombi kwa Stars ishinde.

Lakini pia tukumbuke shabiki wa soka ni mchezaji wa 12 uwanjani hususan timu inapokuwa uwanja wake wa nyumbani.

Na katika kulitambua hilo, tayari Shirikisho la Soka nchini (TFF), limetangaza kiingilio cha chini kabisa cha Sh. 3,000 ambacho ni rafiki kabisa kwa kila mtu mwenye mapenzi mema na Stars kumudu kwenda kuishangilia.

Hivyo, tujitokeze kwa wingi kwenda kuiunga mkono Stars kwani kwa pamoja Afcon 2019 Misri inawezekana wakati huu kikosi hicho cha Amunike kikitarajia kucheza mechi hiyo kama fainali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Adam Fungamwango

# Aiyee asitishwe kuchezea Simba, Yanga

**KWA** sasa kwenye Ligi Kuu ya Tanzania kuna Mtanzania mmoja anaitwa Salum Aiyee, ambaye anashindana na wachezaji kutoka nje ya nchi kwenye kuwania ufungaji bora.

Aiyee anaichezea Mwadui FC akiwa amefikisha jumla ya mabao 15, akiwaburuza kina Meddie Kagere wa Simba aliyecheka na nyavu mara 12 na Heritier Makambo wa Yanga akiwa pia na idadi hiyo ya mabao.

Hawa wawili ni wachezaji kutoka nje ya nchi, lakini Aiyee ni Mbongo.

Kutokana na kufanya vema, tayari anatabiriwa kuwa msimu ujao huenda asiichezee Mwadui na tayari baadhi ya klabu zimeshaanza kumnyemelea. Nimesoma na kusikia baadhi ya wachambuzi wakimuasa kuwa awe makini asijiunge na timu za Simba na Yanga kwa sababu zitakwenda kushusha kipaji chake.

Hii ina maana klabu hizi mbili zina tabia ya kushusha vipaji vya wachezaji wengi nchini.

Binafsi, huu nauita ni uchambuzi, au mtazamo wa kukariri zaidi kuliko uhalisia. Na huu mtazamo huwa unatolewa zaidi mitaani na vijiweni na kuletwa moja kwa moja mezani bila ya kufanyika upembuzi yakinifu.

Na wengi wanaokariri, huwa hawaiingizi Azam kwenye ile tabia wanayodai ni kuua vipaji vya wachezaji kutoka klabu ndogo.

Wao wanaamini wachezaji kama hawa wenye uwezo wakienda Simba au Yanga ndiyo wataua vipaji, lakini wakienda Azam vipaji havifi.

Lakini tumeona mchezaji Mbaraka Yusuph akiwa kwenye ubora wake akienda Azam akapotea, vile vile Waziri Junior akitoka Toto African na kutua Azam, akazimika mpaka alipoibukia Biashara FC ndipo alipoanza kung'ara tena.

Hapa nilitaka kuweka sawa tu kuwa eti mchezaji akienda Azam basi kipaji chake hakifi ila zile timu kubwa tu.

Mimi namshauri Aiyee kama anajiona ana uwezo wa kuchezea Simba, Yanga au hata Azam na wameleta ofa nono basi asisite kwenda kwa sababu zinazotajwa.

Simba na Yanga haziui vipaji vya wachezaji na hazijawahi kufanya hivyo hata siku moja, ila wachezaji wenyewe ndiyo wanaoua vipaji vyao.

Mchezaji anapotoka timu ndogo mikoani kwenda timu kubwa anapaswa aongeze mazoezi mara dufu kwa sababu sasa atakamiwa na kila timu na si kama kule alikotoka.

Wachezaji wengi wa mikoani badala ya kufanya hivyo, wao wanabweteka wanapofika hapo kutokana na kusifiwa na mashabiki, pamoja na pesa wanazopata ambazo ni nyingi kuliko walikotoka.

Baadhi ya wachezaji hujiingiza kwenye starehe, kiburi na kuona wamemaliza kila kitu, hapo kiwango kinaanza kupungua.

Mchezaji anayejitambua kipaji chake hakiwezi kufa atakapojiunga na Simba na Yanga.

Ndiyo maana tumeona kina Shiza Kichuya, Mzamiru Yassin wakitoka Mtibwa Sugar na kwenda Simba, lakini uwezo wao ukaongezeka mara ndufu, mpaka sasa mmoja wao yupo nchini Misri akisakata soka la kulipwa.

Simon Msuva alijiunga na Yanga akitokea Moro United na sasa anacheza soka la kulipwa nchini Morocco.

John Bocco, Erasto Nyoni, Hassan Dilunga, Mohamed Hussein Tshabalala wamejiunga na Simba wakitokea timu mbalimbali na hadi leo ni wachezaji wa kutegemewa. Wangeogopa kwa sababu eti Simba inashusha viwango wasingefika hapo na walipo.

Fesal Salum 'Fei Toto' ametoka Zanzibar, hakuogopa kipaji chake kufa, anaingia Yanga na hadi leo ni kiungo tegemezi kwenye uwezo wa hali ya juu.

Wakati mwingine tunaogopesha wachezaji kwa vitu ambavyo havipo, badala ya kuwapa tahadhari ya wao wenyewe kujiangalia, kujichunga na kujilinda.

Aiyee kama atapata timu na kuridhika nayo kimaslahi asiogope kwenda kwa sababu hapo ndipo maisha yanapoanzia kwa kuwa hata Mbwana Samatta akijiunga na Simba akiwa mdogo, ikiwa na mastaa kama Mussa Hassan Mgosi, Patrick Mafisango, Felix Sunzu, lakini hakuogopa, alipambana na hadi leo tunajua mafanikio yake.

Aiyee anatakiwa ajiogope mwenyewe kwa kufanya vitu visivyotakiwa kwenye maisha ya soka na si kuogopa klabu yoyote ile duniani.

# BARUA/MJADALA

## Tuwatie moyo walimu Minaki

**Mhariri,**

*KATIKA nafasi yangu ya mhitimu wa shule ya sekondari, bado nina kumbukumbu ya siku chache zilizopita, niliposikia sherehe za kuwapongeza walimu na jumuiya ya shule hiyo kwa kazi yao nzuri.*

*Hiyo ni kutokana na kufanya vizuri, zao la kazi yao inaonekana katika matokeo ya wanafunzi kidato cha nne kufanya vyema.*

*Ni jambo linalofurahisha na kutia faraja kwa walio karibu na shule hiyo, hata walio mbali. Hiyo ni kwa sababu katika siku za karibuni kumekuwapo na malalamiko katika sehemu mbalimbali nchini, kulaumu udhaifu wa kitaaluma katika shule mbalimbali.*

*Nikirejea Minaki, shule hiyo tangu zama hizo za ukoloni ikiwa ni aina ya seminari, ina historia ya kufanya vizuri sana katika masomo ngazi zote, kidato cha nne na kidato cha sita.*

*Kuna baadhi ya miaka iliyopita, kumekuwapo na kilio na malalamiko kuhusu Minaki kufanya vibaya kitaaluma, jambo lililozua kilio na malalamiko mengi kuhusiana na hilo.*

*Nashukuru kusikia malalamiko hayo ya kujikwaa katika kiwango cha kitaaluma, yamefanyiwa marekebisho, hata shule ikisimama pazuri kitaaluma.*

*Pia kutoka kwingineko ambako kuna vilio hivyo, ni nafasi nzuri wahusika wakafunga safari kwenda kudodosa kupata maarifa ya uhakika, kuhusiana na chanzo cha ushindi na mafanikio hayo ya kitaaluma Minaki.*

*Kwa lugha rahisi faida hiyo ya ushindi utapanuka kwa ujuzi kufika mbali. Lakini, kupitia usemi, kila penye mafanikio ni kwamba nyuma yake kuna wanaochangia mafanikio yake.*

*Tutafakari namna ya kuwatia moyo zaidi, tena tukitambua hasa ndiko iliko katika wilaya ambayo mbunge wake, ndiye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tamisemi), Suleiman Jafo.*

**Hazadi Petro, Mkuranga.**

## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Hongera Simba, lakini jipangeni ugenini




**Na Adam Fungamwango**

**WAPENZI** wa michezo nchini hususan, wanachama na mashabiki wa Simba wamekuwa na furaha baada ya timu yao kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba imeingia kwenye hatua hiyo baada ya kuichapa AS Vita kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kwa mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi, Jumamosi.

Kwenye Kundi D, Simba imefanikiwa kusonga mbele baada ya kujikusanyia jumla ya pointi tisa ikiwa nyuma ya Al Ahly ya Misri ambayo imeongoza kundi.

Kilichoisaidia Simba kusonga mbele ni wastani mzuri wa kushinda mechi za nyumbani, Uwanja wa Taifa.

Ina asilimia 100 ya kushinda mechi ikiwa nyumbani kwa kushinda mechi zote, kuanzia dhidi ya Mbambane Swallow mabao 4-1, Nkana FC mabao 3-1, JS Saoura mabao 3-0, Al Ahly bao 1-0 na AS Vita mabao 2-1.

Pamoja na rekodi hiyo nzuri, lakini timu hiyo hiyo ina udhaifu mkubwa inapocheza mechi zake za ugenini. Simba ina asilimia zaidi ya 90 ya kupoteza mechi ikicheza nje ya nchi.

Mechi pekee ambayo ilishinda ikiwa ugenini ni dhidi ya Mbabane Swallow iliposhinda mabao 4-0 nchini Swaziland au Eswatini kama inavyojulikana sasa.

Mechi zote zilizobaki imepokea vipigo dhidi ya Nkana mabao 2-1, mabao 5-0 dhidi ya AS Vita na pia Al Ahly na ikafungwa mabao 2-0 dhidi ya JS Saoura.

Hii inaonyesha kuwa timu hiyo bado ina matatizo makubwa inapokwenda kucheza ugenini.

Wawakilishi hao wa Tanzania wanapaswa kupongezwa kwa kuweza kuliweka jina la nchi kwenye ramani nzuri ya soka na sasa tutakuwa tunaangaliwa kama nchi yenye uwezo mzuri wa kutandaza kabumbu, lakini pia hata klabu zetu zitakuwa hazichukuliwi poa zinapokwenda kucheza na timu nyingine za nje.

Hata hivyo, kama Simba inataka kusonga mbele zaidi kwenye michuano hiyo ilichukulie suala la kutoshinda mechi zake nje ya nchi au kuruhusu mabao mengi kama changamoto ambayo inapaswa ifanyiwe kazi na benchi la ufundi likiongozwa na Mbelgiji, Patrick Aussems.

Kocha huyo na wenzake sasa wakae chini na kuangalia ni kitu gani kinachosababisha wachezaji wake wasiweze kucheza kwenye viwango vya kawaida wakiwa ugenini?

Ni kwa sababu tayari Simba inakwenda kucheza mechi ya robo fainali na ili isonge mbele inahitaji sasa isiruhusu kufungwa ugenini, au hata kama ikipoteza lakini isiwe kwa idadi kubwa ya mabao kama tulivyoshuhudia ugenini dhidi ya AS Vita na Al Ahly.

Hii sasa ni ligi tena ila ni mtoano na timu hazihesabiani tena pointi bali idadi ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Kama Simba itaendelea na udhaifu huu wa kutoweza hata kujitutumua kutoa sare ugenini au kuruhusu idadi kubwa ya mabao, basi inawezekana kabisa hapa ilipofika itakuwa ni mwisho wao.

Kwa sababu itafungwa mabao mengi ugenini na kushinda machache nyumbani, hivyo itakuwa imetolewa kwenye mashindano hayo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Timu zote zinazofanya vema kwenye michuano hii hatua iliyofikiwa ni zile zenye uwezo wa kulazimisha sare ugenini au kutofungwa idadi kubwa ya mabao, ikiwamo nayo kuweza kupata hata bao la ugenini ili kurahisisha kazi nyumbani.

Kwa hatua iliyofikia haitakiwi kuendelea kuwa Simba hii tena. Inatakiwa iwe Simba ya kupata mabao mengi nyumbani na kwenda kulazimisha japo sare ugenini.

Kama ikiweza kufanya hivyo, inaweza kufika hadi fainali, lakini kama udhaifu huu hautofanyiwa kazi, basi huenda Simba ikakomea hapo kwenye michuano hii mikubwa kabisa barani Afrika.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED



# 'Elimu ya VVU, TB inahitajika migodini'

Na Shaban Njia, KAHAMA

MKURUGENZI wa Shirika lisilo la Kiserikali la SHDEPH+, Venance Mzuka, amewashauri wachimbaji wadogo wa dhahabu wilayani Kahama mkoani Shinyanga kujenga utaratibu wa kupima afya zao mara kwa mara, hasa ugonjwa wa kifua kikuu (TB) na maambukizo ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa kuwa mazingira yao ya kazi ni rahisi kwao kuambukizwa.

Mzuka alitoa rai hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, akieleza kuwa elimu ya dalili za TB na maambukizo ya VVU inahitajika kwa wachimbaji wadogo ili watambue namna ya kujikinga.

Alidai wachimbaji hao ni rahisi kupata ugonjwa wa TB na maambukizo ya VVU kutokana na mazingira wanayoyafanyia kazi kuwa na mwingiliano wa watu wengi.

Alisema TB huambukizwa kwa njia ya hewa, hivyo ni rahisi kwa makundi yenye mwingiliano mkubwa wa watu kupata ugonjwa huo bila yenyewe kujitambua.

"Wachimbaji wadogo wanafanya kazi zao katika mazingira ambayo si salama, hawana vifaa vya kazi, wanapolipua miamba na usagaji wa mawe ya dhahabu, hutokea vumbi kubwa ambalo huingia kwenye miili yao na kuathiri mapafu na kusababisha wao kuwa na urahisi wa kupata TB," Mzuka alisema.

Meneja Mradi wa TB, Ereneus Nwinuka, alisema ugonjwa huo bado ni changamoto nchini na ndiyo sababu ya kuamua kuweka maofisa katika kila kata ya Halmashauri za Mji wa Kahama na Msalala.

Alisema maofisa wao hao hupita nyumba kwa nyumba kutoa elimu kuhusu chanzo, dalili na madhara ya TB.

Kuhusu VVU, meneja huyo alisema watu wanaoishi na VVU mara nyingi hupoteza maisha kutokana na ugonjwa wa TB kwa kuwa vimelea vya ugonjwa huo hushambulia mapafu na kusababisha kushindwa kufanya kazi yake vizuri.

Kaimu Mkurugenzi wa shirika hilo, Shea Nassoro, alibainisha kuwa mwitikio wa upimaji wa TB ni mdogo katika jamii ukilinganisha na mwitikio wa upimaji wa maambukizo ya VVU kutokana na suala hilo kutopewa uzito.

Nassoro aliwashauri wachimbaji wadogo na watu wanaoishi pembezoni mwa migodi, kujenga utaratibu wa kupima afya zao mara kwa mara ili kujikinga dhidi ya magonjwa nyemelezi ikiwa ni pamoja na TB na maambukizo ya VVU.



Meneja wa kiwanda cha bia cha TBL Arusha, Joseph Mwaikasu (kulia), akitoa maelezo kwa wabunge wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira walipotembelea kiwanda hicho mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bunge lakunwa mradi wa umeme

Na Mwandishi Maalum

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeipongeza serikali kwa kutekeleza mradi wa umeme wa Makambako-Songea (KV 220) ambao umewezesha Mikoa ya Ruvuma na Njombe kupata umeme wa uhakika kutoka Gridi ya Taifa.

Kamati hiyo iliyo chini ya Mwenyekiti Mariamu Ditopile, ilitoa pongezi hizo wilayani Songea mkoani Ruvuma mwishoni mwa wiki, baada ya kukagua utekelezaji wa mradi huo unaohusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo KV 220 kutoka Makambako hadi Songea, ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Makambako, Madaba na Songea na usambazaji umeme katika vijiji 122.

Kabla ya kukagua kituo cha kupoza umeme cha Songea, kamati hiyo ilikagua vituo vya Makambako na Madaba pamoja na njia ya usafirishaji umeme kutoka Makambako hadi Songea, watendaji mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme (Tanesco) wakitoa maelezo ya mradi huo kwa wajumbe wa kamati.

Pamoja na pongezi hizo, Ditopile aliagiza wizara na Tanesco kuhakikisha wanapeleka umeme katika vijiji vyote vilivyopangwa kupelekewa huduma hiyo kupitia mradi huo na kutoruka kijiji chochote ambacho kimepitiwa na mradi.

Kiongozi huyo wa kamati pia aliiagiza wizara na shirika hilo kuhakikisha wanahamasisha wananchi kutumia umeme huo kwa matumizi mbalimbali kwa kuwa mikoa hiyo sasa ina umeme wa kutosha na wa uhakika na serikali inahitaji wateja wengi zaidi ili kuongeza mapato.

Awali, katika kituo kupoza umeme cha Makambako, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alieleza kamati hiyo kuwa mradi huo ulikamilika mwaka 2018 na kazi inayoendelea sasa ni usambazaji wa umeme katika vijiji vya awali 122 na tayari vijiji 105 vimeshaunganishwa nishati hiyo.

Dk. Kalemani aliongeza kuwa mradi huo umetekelezwa na Tanzania kupitia Tanesco kwa kushirikiana na Sweden kupitia Shirika la Maendeleo la Sweden (Sida), ukigharimu Sh. bilioni 216 na kwamba wateja wa awali 22,000 watafaidika na mradi huo.

Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Innocent Luoga, alisema miundombinu hiyo ya usafirishaji umeme (kV 220) imejengwa kwa umbali wa Km 250 na nguzo 711 zimesimikwa.

Aliongeza kuwa kufika kwa umeme wa Gridi ya Taifa katika mikoa hiyo, kumefanya wananchi wahamasike kutumia umeme huo, akibainisha kuwa awali matumizi ya umeme kwa Mkoa wa Ruvuma yalikuwa ni takriban MW tisa, lakini sasa yameongezeka na kufikia MW 11.

# Mbinu kukwepa imani za kishirikina yatajwa

Na Jumbe Ismailly, IKUNGI

MKUU wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, amewataka wananchi wilayani mwake kutumia fursa za kuichumi zilizoko kwenye maeneo yao, kuongeza vipato vyao, akiamini mtu mwenye uchumi mzuri hawezi kuwaza kulogwa.

Katika hotuba yake iliyosomwa na Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Miraji Mtaturu, wakati wa kukabidhi kisima kwa Kitongoji cha Taru, kilichoko kata ya Mang'onyi, wilayani Ikungi mwishoni mwa wiki, Nchimbi alisema ikiwa kipato cha wananchi kitaongezeka, imani za kishirikina zitatoweka katika jamii.

"Sasa ndugu, kipato kizuri kikiwapo, maneno maneno yanatoweka, uchumi ukikua, hauwazi tena kulogwa, ndiyo uzuri wa uchumi," Nchimbi alieleza katika hotuba yake hiyo.

Alisema mkoa wake bado unakabiliwa na changamoto ya baadhi ya wakazi wake kuamini dhana potofu kuwa mwili wa mtu mwenye ualbino ni utajiri, akibainisha kuwa baadhi ya wachimbaji wa madini wanaotaka njia za mkato za kutajirika hutumia viungo vya watu wenye ualbino kuendesha shughuli zao za uchimbaji.

"Yaani unamkuta mtu anahangaika eti achukue kiungo, kiungo gani? Huyo mwenyewe mwenye mwili hajawa tajiri, wewe ukate kiungo tu," alisema.

Awali akitoa taarifa ya mradi huo, Meneja Mkuu Mradi wa Shanta Singida, Philbert Rweyemamu, alisema kisima hicho kimegharimu Sh. milioni 51.5 zilizotumika katika utafiti, uchimbaji na utayarishaji kisima, pampu, kipimo cha usalama wa maji, ujenzi wa miundombinu na mfumo wa umemeja.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Mohamedi Ramadhani, alipongeza Kampuni ya Shanta kwa utekelezaji wa mradi huo na kuahidi kulinda miundombinu yake yote.

**"Sasa ndugu, kipato kizuri kikiwapo, maneno maneno yanatoweka, uchumi ukikua, hauwazi tena kulogwa, ndiyo uzuri wa uchumi," Nchimbi alieleza katika hotuba yake hiyo.**

## Wawekezaji waitwa utalii Kanda ya Ziwa

**Na Mwandishi Maalum**

WIZARA ya Maliasili na Utalii imeanza uhamasishaji kuwavutia wawekezaji watakaosaidia kuwapeleka watalii maeneo ya Kanda ya Ziwa baada ya serikali kuweka miundombinu wezeshi ya utalii katika maeneo hayo.

Hamasa hiyo imetolewa baada ya serikali kuyapandisha hadhi mapori ya Akiba ya Burigi, Biharamulo, Kimisi, Ibanda na Rumanyika kuwa hifadhi za taifa.

Akizungumza kwenye ufunguzi wa mkutano wa siku moja uliofanyika jijini Mwanza kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na wawekezaji kutoka maeneo mbalimbali nchini mwishoni mwa wiki, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alisema sekta binafsi ni injini ya utalii nchini. Alisema mkutano huo ni muhimu kwa kuwa wizara inapata nafasi ya kuwaeleza wawekezaji fursa mbalimbali zinazopatikana katika ukanda huo na wawekezaji kueleza changamoto zinazowakabili.

Alisema sekta binafsi itakuwa na kila sababu ya kuwekeza katika ukanda huo baada ya serikali kuendelea kuweka mazingira rafiki kwa uwekezaji.

Aliitaja baadhi ya miundombinu wezeshi iliyowekwa na serikali kuwa ni pamoja na ujenzi wa barabara, ukarabati wa viwanja wa ndege. Kanyasu alisema Tanzania imekuwa ikifanya vizuri kwenye shughuli za uhifadhi, lakini katika bado kuna changamoto kwenye kuvutia watalii wengi zaidi kutembelea hifadhi zilizopo nchini, hivyo jitihada za makusudi zinahitajika.

"Tuna vivutio vya utalii vingi, lakini ukilinganisha na idadi ya watalii tunaopata, hailingani kabisa," Kanyasu alisema.

Mwandaaji wa mkutano huo ambaye pia ni Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Adolf Mkenda, alisema kupitia mkutano huo, wanaamini watachagiza idadi ya watalii kuongezeka kwa kutembelea vivutio vya utalii vinavyopatikana katika ukanda huo.

Alisema mkutano huo ni sehemu ya mkakati wao wa kutawanya fursa za uwekezaji wa sekta ya utalii nchi nzima. Mkenda wanatarajia kuandaa mkutano mwingine kwa ajili ya Kanda ya Kusini katika Mji wa Iringa na baadaye watawakutanisha wawekezaji mkoani Pwani ili kuendelea kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta ya utalii.

Akichangia hoja kwenye mkutano huo, Mwenyekiti wa Chama cha Wasafirishaji Watalii (Tato), Willy Chamburo, aliiomba serikali iangalie itakavyojizuia kubadili sera kila mara katika masuala ya utalii kwa kuwa kunachangia kuwakatisha tamaa wawekezaji.

Alisema wawekezaji wanataka kuwekeza mahali ambako wana uhakika wa kupata faida itayowasaidia kujiendesha kibiashara na kulipa kodi stahiki za kiserikali.

Katika mkutano huo, wakuu wa mikoa yote ya Kanda ya Ziwa wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, walikuwa ni miongoni mwa washiriki.

# Aagiza kuswekwa ndani wanywaji pombe asubuhi

**Na Friday Simbaya, IRINGA**

DIWANI wa Kata ya Mwanagata katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Ngugvu Chengula, ameagiza kukamatwa watu wote wanaokunywa pombe za kienyeji nyakati za kazi.

Amesema anaamini ulevi kupita kiasi ni miongoni mwa mambo yanayochangia kukwamisha maendeleo katika jamii, akieleza kuwa amekuwa akisikitika kuona baadhi ya wananchi wanakunywa pombe asubuhi badala ya kufanya kazi za kuwaongeza kipato.

Chengula alitoa agizo hilo jana alipozungumza na wamiliki wa nyumba katika kata yake alipohitaji kujua idadi ya nyumba na wakazi walioko katika kila nyumba. Alisema atawakamata watu wote wanaokunywa pombe kwenye vilabu nyakati za kazi kwa kuwa wanakwamisha maendeleo.

Diwani huyo aliwataka wenyeviti na watendaji wa mitaa yote kuhakikisha vilabu vya pombe vyote vinafunguliwa kuanzia saa 10 jioni baada ya watu kumaliza kazi zao.

Alisema wamiliki wa vilabu hivyo wanapaswa kuzingatia agizo hilo vinginevyo wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa kuwa ndiyo chanzo cha kuwa na vibaka na kurudisha nyuma maendeleo ya wananchi na serikali kwa ujumla.

Alidai kuwa kata yake hiyo inaongoza Manispaa ya Iringa kwa kuwa na idadi kubwa ya watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU). Halmashauri hiyo ina kata 18.

Alidai kasi ya maambukizo ya VVU inasababishwa na ngono zembe kutokana na unywaji holela wa pombe za kinyeji na matumizi ya dawa za kulevya.

Chengula pia alisema atashirikiana na wataalamu wa Manispaa ya Iringa kufanya operesheni ya nyumba kwa nyumba kukagua vyoo na ikibainika nyumba haina choo, hatua stahiki zitachukuliwa dhidi ya wahusika.



Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Bima wa Benki ya NBC, Benjamin Nkaka (katikati), akimkabidhi pikipiki mmoja wa washindi wa shindano la Shikandinga Mkoa wa Dar es Salaam kwa upande wa wanawake, Habiba Salum, wakati wa uzinduzi wa shindano hilo ambalo NBC ni mdhamini mkuu lililofanyika mkoani humo, mwishoni mwa wiki. Kulia ni Ofisa Mikopo wa NBC, Clara Jackson. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Msako nguo za ndani za mtumba washika kasi

**Na Mwandishi Wetu**

MSAKO wa kuondoa nguzo za ndani za mtumba umeshika kasi Dar es Salaam baada ya maofisa wa Shirika la Viwango (TBS) kuzidisha operesheni hiyo kwenye Soko la Karume jijini.

Operesheni ya kuondoa nguo hizo ilifanyika mwishoni mwa wiki chini ya usimamizi wa Jeshi la Polisi, lengo likiwa ni kuhakikisha nguo hizo hazitumiwi na Watanzania kutokana na kuwa na madhara kiafya.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa msako wa kuondoa nguo hizo sokoni, Mkaguzi wa TBS, Emmanuel Simon, alisema hatua hiyo ni mwendelezo wa mkakati wa shirika wa kuondoa nguo hizo nchi nzima.

Alisema miongoni mwa malengo ya uwapo wa shirika hilo ni kulinda afya za walaji, hivyo wanaondoa nguo hizo kwenye soko kwa kuwa zina madhara.

Aliyataja baadhi ya madhara ya kiafya yanayosababishwa na nguo hizo kuwa ni magonjwa ya ngozi ikiwamo kansa.

"Kwa hiyo, tunatoa wito kwa Watanzania, wasipende kuvaa nguo za ndani za mitumba, zina madhara, ndiyo maana tunaziondoa," alisema.


Simon pia aliwataka wafanyabiashara kuachana na uingizaji wa nguo za ndani za mtumba ili kuepuka hasara. Alisema baadhi ya Watanzania wanavutiwa na nguo hizo kutokana na unafuu wa bei, lakini madhara yanayotokana nazo ni makubwa.

Alisema nguo hizo zimekuwa zikiingizwa nchini na wafanyabiashara wasio waaminifu kupitia njia zisizo rasmi, lakini wananchi wakizikataa kuzinunua, waingizaji wake wataacha.

Alisema msako unaendeshwa na maofisa wa shirika hilo nchi nzima kutokana na matakwa ya kisheria. Tangazo la kupiga marufuku nguo hizo lililotolewa kwenye vyombo vya habari na sasa operesheni itekelezwa kwa kuziondoa kwenye soko.

"Utekelezaji huu ni kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Viwango ya Mwaka 2009 inayozuia matumizi ya nguo za ndani za mitumba. Licha ya unafuu wa gharama za upatikanaji wa nguo za mitumba nchini, serikali kupitia shirika letu imepiga marufuku biashara ya uuzwaji wa nguo hizo, kwa maana ya soksi, sindiria na nguo za kulalia kwa sababu zina madhara kwa mtumiaji," alisema.

HABARI ARUSHA



# Watafiti dawa za binadamu kukitumia Chuo cha Mandela

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WATAALAMU na watafiti wa dawa za binadamu kutoka ndani na nje ya Bara la Afrika wamekubaliana kukitumia Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela kuandaa programu za mafunzo ya shahada ya uzamili katika utafiti wa dawa za binadamu.

Wamesema programu hiyo itaendeshwa kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Purdue cha Marekani.

Makubaliano hayo yalifikiwa baada ya kongamano lao lililofanyika chuoni hapo mwishoni mwa wiki.

Akizungumzia makubaliano hayo, Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Emmanuel Luoga, alisema wanatarajia kuanza kuzalisha wataalamu wa utafiti wa dawa za binadamu baada ya miaka miwili kuanzia sasa.

Mkurugenzi Mkuu wa Bohari ya Dawa (MSD), Laurian Mwigambwa, alisema tatizo la ukosefu wa wataalamu na viwanda vya kutengeneza dawa za binadamu ni kubwa zaidi katika nchi za Afrika.

Kutokana na changamoto hiyo, Mwigambwa alisema dawa nyingi za binadamu katika nchi hizo zinatengenezwa Ulaya na Marekani. Akizungumza katika kongamano hilo, mtaalamu kutoka Chuo Kikuu cha Purdue, Stephen Byrn, alisema mpango huo ukikamilika, utakuwa mkombozi mkubwa kwa nchi za Afrika.

Mada kuu katika kongamano hilo ilikuwa namna ya kuandaa wataalamu wa kutosha wa utafiti na kutengeneza dawa za binadamu.




Mwenyekiti wa chama cha wachimbaji madini Mkoa wa Manyara (Marema), tawi la Mirerani wilayani Simanjiro, Shwaibu Mushi, akizungumza kuhusu wachimbaji kutoa taarifa za migodi yao juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Vijana wafundishwa mbinu ubunifu miradi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MRADI wa Majukwaa ya Vijana umetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana 28,000 wa Kata za Lemara, Unga Ltd na Sokoni One katika Jiji la Arusha ili kuwawezesha kubuni miradi itakayowakwamua kiuchumi.

Akizungumza wakati wa mashindano ya maonyesho ya bidhaa kutoka kwa vijana hao, Ofisa Tawala Msaidizi wa Taasisi ya Arusha Municipal Community (AMCF), Anna Mushi, alisema mafunzo hayo yametolewa kupitia majukwaa ya vijana wa kata hizo kwa lengo la kuwasaidia kujikwamua kiuchumi.

"Tumewafundisha njia za uhakika za kuzalisha bidhaa bora ili waweze kujiajiri na kukuza uchumi wao na wa taifa kwa ujumla," Mushi alisema.

Aliongeza kuwa wametoa mafunzo ya uongozi, utawala bora, namna ya kushiriki katika shughuli za kiserikali kwa ajili ya maendeleo, kutambua fursa zilizoko kwenye jamii na kushiriki katika ngazi za kutoa uamuzi.

Alisema vijana hao wamenufaika kupata elimu ya ujarisiamali na masoko, biashara na ubunifu ili wakuze na kuongeza vipato vyao vya kiuchumi. "Tunawahamasisha vijana wajasiriamali wasitegemee kuajiriwa tu, husani wale walioko vyuoni, tunawashauri kujiunga katika makundi mbalimbali kwa ajili ya kuanzisha viwanda vidogo," alisema.

Ofisa Idara ya Maendeleo ya Jamii kutoka Halmashauri ya Jiji la Arusha, Hanifa Ramadhani, alisema katika bajeti ya mwaka 2018/19, halmashauri hiyo ilitoa mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 665 kwa vikundi 118 kutoka kata 25 za Jiji la Arusha.

Alisema maelekezo ya serikali kila mwaka wa bajeti, kila halmashauri inatakiwa kutenga asilimia 10 ya mapato kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

"Mwongozo wa serikali katika asilimia hizo 10 ya mapato tuliyokusanya tunatoa asilimia nne kwa vijana, nne zingine kwa wanawake na asilimia mbili kwa walemavu," alisema.

Wakizungumza kwa niaba ya vijana wengine walioshiriki katika maonyesho hayo, Ibrahimu Kikoti na Sara Mosess, walisema kupitia mafunzo hayo, wameongeza maarifa ya kuwa wabunifu wa kuchangamkia fursa kwa kuzalisha bidhaa bora na kutafuta masoko ya uhakika.

"Kilichosababisha mimi kuingia katika ujasiriamali, ni mafanikio na maendeleo yanayokuja baada ya watu kuchukua jukumu la kujiajiri, inawasaidia kukuza kipato kwa kuwa kazi anayoifanya ni yake, hivyo ataimudu kwa njia yoyote," alisema.

# Wazee wa kimila wamwita Lukuvi

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WAZEE wa kimila kutoka Kata ya Majengo wilayani Arumeru, wamemwomba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, kuingilia kati mgogoro wa mpaka kati ya vijiji vya Majengo na Patanumbe vilivyoko Kata ya Makiba.

Wamesema mgogoro huo wa zaidi ya miaka 10, utasababisha kuvunjika kwa amani kwenye eneo hilo.

Wakizungumza katika mkutano wa hadhara mwishoni mwa wiki, mwenyekiti wa wazee hao, Yesse Kamunduli na mwenzake Saitoti Kohoni, waliomba Wizara ya Ardhi kuumaliza mgogoro huo.

Walidai mgogoro huo ulianza baada ya wananchi wa Kijiji cha Patanumbe kuvamia Kitongoji cha Majengo Dipu kilichoko Kata ya Majengo na kukichukua bila kufuata taratibu za kisheria.

"Kitongoji cha Majengo Dipu kipo ndani ya Kijiji cha Engatani, Kata ya Majengo tangu nchi hii ilipopata uhuru wake, mipaka iliwekwa kisheria na inajulikana kwa vipindi vyote tulipoishi hapa, lakini ndugu zetu kutoka Patanumbe wamevuka mipaka na kuingia katika eneo letu na hawataki kuitambua mipaka iliyowekwa kisheria," Kamunduli alidai.

"Kwa kweli, kitu ambacho kimetushangaza ni hawa ndugu zetu wanataka kulimega eneo letu la Kitongoji cha Majengo Dipu na kuliingiza kwao, sisi hatutaki shari na mtu yeyote, hivyo tunamwomba Waziri wa Ardhi (Lukuvi) kutusaidia kutatua mgogoro huu ili usije kuleta madhara makubwa kwa wananchi wa pande hizi mbili," Kohoni alisema.

Aliongeza kuwa katika kushughulikia mgogoro huo, awali aliyekuwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Alexander Mnyeti (sasa Mkuu wa Mkoa wa Manyara), alituma timu ya wataalamu wa ardhi kutatua mgogoro huo na kwa kiwango kikubwa walifanikiwa kubainisha mipaka halali iliyowekwa tangu mwanzo wa kuanzishwa kwa kata na vijiji hivyo.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, baada ya hali ya sintofahamu kujirudia katika eneo hilo, pia alituma wataalamu wa ardhi kwa mara nyingine kupima upya eneo na kuonyesha mipaka ilivyokuwa tangu mwanzo na ramani ilionyesha kama mipaka ilivyowekwa awali wakati wa mgawanyo wa vijiji hivyo.

"Tunawashukuru sana viongozi hawa waliojitahidi kushughulikia mgogoro huu, lakini kinachotusikitisha ni kwamba wataalamu walewale waliokuja kubainisha mpaka huu katika utawala wa Mnyeti na Muro ndiyo hao walikuja wiki iliyopita kubatilisha mipaka hiyo, bila ya kushirikisha pande mbili.

"Suala hili lisipodhibitiwa mapema, linaweza kuleta uvunjifu wa amani hivyo, ombi letu kwa serikali, Waziri Lukuvi afike eneo hili na kutatua mgogoro huu," Kamunduli alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Engatani, Edward Siria, alisema kwa kipindi cha miaka mitano ya mgogoro huo, baadhi ya wananchi wamechomewa makazi yao na kijana mmoja wa kijiji chao kupoteza maisha kutokana na kukatwa kwa mapanga.





# DC, vigogo wanne matatani Takukuru

**Na Godfrey Mushi,** HAI

VIGOGO watano wa serikali, akiwamo mkuu wa wilaya mstaafu, wanaotuhumiwa kuchepusha ekari 12 za ardhi kwenye eneo la maendelezo ya viwanda la Weruweru wilayani Hai mkoani Kilimanjaro, wameingia matatani baada ya majina yao kukabidhiwa rasmi kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Vigogo hao wanadaiwa kujigawia ekari mbili kila mmoja baada ya kufanikiwa kuliondoa eneo hilo kwenye eneo lililotengwa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa viwanda.

Taarifa za kuanza kwa uchunguzi dhidi ya viongozi hao zilithibitishwa na Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya mwishoni mwa wiki.

Wanaochunguzwa ni pamoja na aliyekuwa Mkurugenzi wa wilaya hiyo na Mkuu wa Wilaya za Monduli na Ulanga kwa vipindi tofauti, Mweka Hazina wa zamani wa wilaya hiyo na watumishi watatu wa wilaya hiyo. Ole Sabaya tayari ameagiza uchunguzi dhidi ya vigogo hao ufanyike ndani ya siku saba, huku akiwataka kurejesha ardhi hiyo waliyoimega.

"Tunataka hayo maeneo, tunataka hizo ekari 12 zikiwa zimenyooka. Mkurugenzi (Yohana Sintoo) unatafuta ekari 120 za kujenga soko, lakini watu wanakalia na wanahangaika kuuza," alisema.

Awali, Ofisa Ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Jackob Muhumba, alimweleza Ole Sabaya kwamba katika makisio ya bajeti ya halmashauri hiyo kwa mwaka ujao wa fedha (2019/20), alipendekeza kutengwa bajeti ya Sh. milioni 247 kwa ajili ya upimaji ili kupunguza migogoro, lakini akaishia kuonekana kituko.

Muhumba alidai alipendekeza bajeti hiyo ili kutatua migogoro ya ardhi na kulipa fidia kwa wananchi ambao wanadai lakini hawajalipwa kutokana na ufinyu wa bajeti.

Katika kikao kazi cha watendaji wa wilaya hiyo mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mtendaji wa wilaya hiyo (Sintoo), aliagiza watendaji wote wa kata kuorodhesha migogoro ya ardhi katika maeneo na kuanza kuitatua.



Wananchi wa Mtaa wa Kwaminchi uliopo katikati ya Jiji la Tanga wakiwaokoa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Horten waliopata ajali baada ya basi walilokuwa wakisafiria juzi, kugonga treni na kuburuzwa umbali wa mita 50, watu wawili wamefariki na wengine 30 kujeruhiwa. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

## Wafundwa kukwepa jela makosa ya kimtandao

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA) imeanza kutoa mafunzo kwa wanafunzi ili kupunguza kasi ya matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii.

Maofisa wa mamlaka hiyo wameanza kutoa mafunzo hayo kwa wanafunzi wa shule kongwe za serikali wakiwahimiza kutumia mitandao hiyo kwa faida, badala ya kuingia katika mtego wa kuvunja Sheria ya Makosa ya Kimtandao.

Ofisa Mkuu Mwandamizi wa Idara ya Leseni na Udhibiti wa Mawasiliano wa TCRA, Cecilia Mkoba, alisema mwishoni mwa wiki kuwa wameona kuna haja ya kutoa mafunzo hayo ili kupunguza watumiaji wasiozingatia maudhui ya Sheria ya Makosa ya Kimtandao.

Mafunzo hayo katika Mkoa wa Kilimanjaro yameanzia Shule ya Sekondari ya Ufundi Moshi ambayo ni moja ya shule kongwe kitaifa zilizowika miaka ya 1980 hadi 1990.

Mbali na kutoa mafunzo hayo, mamlaka hiyo imewataka watoa huduma za mawasiliano nchini, kuzingatia mahitaji ya mlaji na sheria wakati wa kutoa huduma zao.

# Bunge lajitosa mgogoro kati ya shirika, kiwanda

**Na Paul William,** MOSHI

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira imeingilia kati mgogoro wa ardhi kati ya Shirika la Reli na Kiwanda cha Bia cha Serengeti.

Baada ya kuzuru katika eneo lenye mgogoro, kamati hiyo imeagiza serikali isitishe mara moja bomoabomoa inayolenga kuruhusu kuanza kwa ujenzi wa reli ya kaskazini.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Suleiman Sadiq, alisema yapo mambo matatu ambayo wamekuwa wakijiuliza ikiwa ni pamoja na kesi iliyofunguliwa mahakamani na wananchi kuzuia nyumba zao kuvunjwa.

Kiongozi huyo wa kamati alisema uongozi wa Kiwanda cha Serengeti pia umekataa kubomolewa sehemu ya kiwanda chake, huku kamati ikionyeshwa barua ya Shirika la Reli inayotaka kubomolewa kwa kiwanda hicho na makazi ya watu yaliyoko katika eneo hilo.

Alisema suala la wamiliki wa kiwanda hicho na wananchi mpaka sasa kutokuwa na barua maalum inayoonyesha kuwa mgogoro huo umeisha, watalibeba kwenda bungeni.

"Mgogoro huu sisi kama kamati tumeona unauhitaji wa haraka wa kutatuliwa kwa sababu unashirikisha wawekezaji wawili, mwekezaji wa ndani na mwekezaji wa nje.

"Sasa, wawekezaji hawa tunawakatisha tamaa kwa namna moja au nyingine na nia ya kamati yetu ni kuunga mkono juhudi za Rais Dk. John Magufuli katika kuijenga Tanzania ya viwanda," alisema.

Sadiq aliongeza kuwa Serengeti ni miongoni mwa viwanda ambavyo ni walipaji wazuri wa kodi nchini, kikiwa pia miongoni mwa viwanda vilivyobinafsishwa.

"Kazi yetu kubwa sisi kama Bunge ni kuishauri serikali baada ya kuona mgogoro huu watatoa taarifa yao bungeni na kutoa ushauri kuhusu mgogoro huo kumalizika mapema na kwa amani bila kukatisha tamaa wawekezaji nchini," alisema.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, alisema Kiwanda cha Serengeti ni kiwanda cha pili kwa utoaji huduma bora za pombe nchini.

Alisema changamoto inayokikabili kiwanda hicho ni mgogoro wa ardhi kati yake na Shirika la Reli, lakini akasisitiza kuwa uwekezaji uliofanyika katika kiwanda hicho ni mkubwa na una tija kubwa kwa taifa, hivyo iko haja kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kukaa meza moja na Wizara ya Ujenzi ili kutatua changamoto hiyo.

"Niwatoe hofu wawekezaji nchini, serikali inatambua mchango wao na ipo kwa ajili ya kuangalia maslahi yao mapana katika kukuza uchumi. Miongoni mwa wawekezaji wanaofanya vizuri ni wa Kiwanda cha Bia cha Serengeti," Manyanya alisema.

Nipashe
# Spotika
NIPASHE JUMATATU MACHI 18, 2019



SIMBA ILIVYOITEKA AFRIKA KIPIGO AS VITA U/TAIFA UK.18

## KOMBORA...



Winga wa Manchester City, Leroy Sane, katika harakati za kujaribu kufunga kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la FA dhidi ya Swansea, ambayo walishinda 3-2. **PICHA: MTANDAO**

### ISIKUPITE

USHINDI wa jumla wa mabao 10-2 Manchester City iliyoupata kwenye hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Schalke, ni wa kipekee kwa hivi karibuni, timu ambayo imewahi kupata ushindi wa jumla mkubwa katika hatua hiyo ya 16-bora ni Bayern Munich ambayo ilisonga mbele kwa jumla ya tofauti ya mabao 12-1 dhidi ya Sporting CP msimu wa 2008-09.




# SABABU RONALDO KUIFUNGA ATLETICO

**TURIN,** Italia

KILA wakati uliopita unaonekana kuwa mzuri zaidi kwa Cristiano Ronaldo. Anaweza kuwashtua wengi kwa kusahihisha makosa yaliyopita na kufanya maajabu. Ana umri wa miaka 34, lakini bado anaonyesha kuwa unaweza kumtegemea katika jambo muhimu.

Vichwa vyake viwili na bao la penalti vilimwezesha kufunga 'hat-trick' yake ya kwanza akiwa na klabu ya Juventus. Lakini jambo zuri zaidi ilitokea wakati Bianconeri hao walipokuwa wakihitaji mno msaada wake.

Walipoteza kwa Atletico 2-0 kwenye mchezo wa kwanza uliopigwa pale Madrid nchini Hispania. Lakini wakaweza kupindua matokeo dhidi ya timu hiyo ya kocha Diego Simeone.

Na mabao yake ndiyo yaliyoiwezesha Juventus kufuzu robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ronaldo amefunga mabao 24 katika mechi 33 dhidi ya Atlético Madrid na ilikuwa 'hat-trick' yake ya nane kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Yeye ndiye mchezaji pekee aliyeifunga Atletico 'hat-trick' nne.

Hapa tunaangalia sababu tatu zinazomfanya Ronaldo awapatie zaidi Atletico Madrid...

**1. Anajua kujipanga**

Cristiano Ronaldo anaendelea kuwa mmojawapo wa wafungaji bora zaidi katika kizazi cha sasa cha wanasoka. Inashangaza sana kumwona anaweza kufanya kazi hiyo sasa wakati akiwa na umri wa miaka 34, wakati ambao miguu yake haina kasi na yenye nguvu kama ilivyokuwa mwanzo. Lakini Mreno huyo anabakia kuwa mmoja wa waviziaji bora duniani, lakini kwa sababu nzuri.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or anajua kujipanga na ana akili ya kujua wapi sehemu sahihi ya kuvizia mpira, na ndicho alichowafanyia Atletico Madrid, kwa kuwa walishinda kumlinda. Kutoka kwenye nafasi ya mpira kumruhusu awe mahali pazuri, kwa wakati mzuri, kuweka mpira ndani ya wavu.

**2. Nafasi nyingi**

Kiukweli hii ni sababu rahisi zaidi. Unapomlisha mipira mchezaji bora duniani kama Cristiano Ronaldo, nafasi nyingi ataweza kufunga. Makosa ya Atletico Madrid ilikuwa ni kukaa nyuma na kulinda lango, kitu ambacho kiliwawia vigumu zaidi kwao.

Kwa mfano, Cristiano hakuwa kwenye kiwango chake katika mchezo wa kwanza, kwa sababu Juventus waliingia kwa nia ya kujilinda zaidi. Bianconeri hao hawakuwa wakitumia mipira yao ili kupata mipira ndani ya eneo la hatari la Atletico Madrid walikuwa na haraka ya kufunga. Hilo lilimfanya Ronaldo kuwa peke yake mbele na kukosa mtu wa kumlisha mipira.

Mambo yalikuwa tofauti katika mchezo wa pili, kwa kuwa Juventus walikuwa wanahitaji ushindi ili waweze kusonga mbele. Kwa hiyo, Ronaldo alifunga katika krosi mbili alizozipata na kuisaidia timu yake kupindua matokeo.

**3. Hamasa**

Ni dhahiri, Atletico Madrid ni waathirika wa zamani wa Ronaldo. Baada ya bao la kwanza walionekana kurudi nyuma na hakukuwa na mpango wowote wa kusukumiza mashambulizi mbele.

Na jinsi mchezo ulivyokuwa unakwenda, wakajikuta wanashindwa kuhimili presha ya Juventus na kujikuta wakifungwa kirahisi.

Wakati huo huo, Cristiano amezoea shinikizo. Amefunga 'hat-trick' nyingi huku nyuma na kuweza kupindua matokeo. Aliwahi kufanya hivyo dhidi ya Wolfsburg wakati akiwa Juventus. Alikuwa na njaa na aliamua kufanya kile kilichowezekana kuisaidia timu yake.

Ingawa Juventus ilipoteza mabao licha ya kufunga mabao matatu Santiago Bernabeu, ni dhahiri kwamba kuwasili kwa Cristiano kuliongeza nafasi yao, na kuwafanya kuwa na uhakika zaidi wa kupata ushindi na kurudi tena mchezoni kama ilivyotokea kwenye mchezo huo na wakafuzu robo fainali.

**JE, WAJUA?**

ATLETICO Madrid inakuwa timu ya nne kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano kushinda mechi ya mkondo wa kwanza kwa mabao 2-0 nyumbani, lakini ikashindwa kusonga mbele hatua inayofuata.

# MICHEZO

## NJE YA UWANJA




## BINGWA UEFA HUYU HAPA

**PARIS,** Ufaransa

MIAMBA minne; Barcelona, Juventus, Manchester City na Liverpool - iliyobaki Ligi ya Mabingwa Ulaya kati ya nane, ndiyo inayopewa nafasi kubwa ya kutinga nusu fainali, wakati huu zote zikiwa zimekwepana katika hatua hii ya robo fainali, kwa mujibu wa mchambuzi Simon Gleave.

Juventus imekadiriwa kuwa na asilimia 85 ya nafasi ya kutinga nusu fainali kwa kuitoa Ajax, wakati Barcelona ikiwa na makadirio ya asilimia 78 kuitoa Manchester United na kutinga hatua hiyo.

Manchester City yenyewe inapewa asilimia 71 ya nafasi ya kutinga nusu fainali kwa kuifurumusha Tottenham Hotspur, huku Liverpool ikiwa na asilimia 68 ya kuitoa FC Porto na kutinga nne bora.

Hata hivyo, Barcelona inaongoza kwa kupewa asilimia 38 ya kutwaa ubingwa huo ikifutiwa na Juventus asilimia 24 wakati Manchester City ikipewa asilimia 19 kwa kumaliza msimu na ubingwa huo kisha Liverpool (asilimia 10). Aidha, nafasi ya timu kutoka England kutwaa ubingwa huo imeshuka kwa asilimia 35.



Beki wa KMC, Ally Ally, akijaribu kumzuia straika wa Yanga, Heritier Makambo (kulia), asilete madhara kwenye goli lake. Beki hiyo alijifunga na Yanga kuondoka na ushindi wa mabao 2-1.

# WAKALI 10 WA KUJIFUNGA BARA

**Na Adam Fungamwango**

KABLA ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya Simba dhidi ya AS Vita, habari kuu ya soka ilikuwa ni beki wa KMC Ally Ally alivyojifunga bao kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu yake dhidi ya Yanga.

Ally alijifunga bao Machi 10 na kuifanya Yanga kuondoka na ushindi wa mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Taifa.

Tatizo halikuwa kujifunga, ila wengi walikwenda nyuma na kukutana na rekodi safi ya kuifungia Yanga mabao, huku akiwa anaichezea timu nyingine.

Rekodi zilionyesha kuwa Machi 12 Ligi Kuu msimu uliopita, Ally Ally alipojifunga bao dakika ya saba, kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, Yanga ikiichapa Stand United mabao 3-1.

Siku aliyoifungia KMC ilikuwa ni Machi 10, hivyo zilisalia siku mbili tu atimize mwaka mmoja tangu aifungie Yanga bao akiwa Stand, lakini siku mbili kabla akajifunga tena.

Msimu huu si Ally Ally aliyejifunga kwa kuwa kuna mlolongo wa wachezaji wengi walioweka kambani mpira kwenye goli lao wenyewe. Nao ni hawa hapa...

**1. Tumba Swedi-(Coastal vs Ruvu Shooting)**

Mchezaji wa kwanza kabisa kujifunga kwenye Ligi Kuu msimu huu ni Tumba Swedi wa Coastal Union. Aliweka rekodi hiyo Septemba 22, mwaka jana, timu yake ikicheza dhidi ya Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani. Hilo likawa bao pekee, Coastal ikilala kwa bao 1-0.

**2. Lameck Daniel-(Biashara vs Mwadui)**

Beki wa Biashara FC ya Mara, aliwafungia wapinzani Mwadui bao la kwanza kwenye mechi iliyochezwa Oktoba 7, mwaka jana katika Uwanja wa Karume mjini Musoma. Bao hilo la kujifunga liliwapa nguvu Mwadui kiasi cha kuongeza la pili lililofungwa na Ibrahim Irakoze, Biashara ikafa nyumbani 2-0.

**3. Erick Murilo-(Simba vs Stand United)**

Mwingine ni Erick Murilo. Huyu ni beki wa Stand United. Oktoba 21, mwaka jana kwenye Uwanja wa Taifa, mechi ya mzunguko wa kwanza, Simba ilishinda mabao 3-0. Emmanuel Okwi alifunga moja na Clatous Chama moja. Murilo alijifunga dakika ya 77 na kuipa Simba bao la tatu.

**5. Bakari Mwamnyeto-(Coastal vs Mbeya City)**

Ilikuwa ni Desemba 8, mwaka jana kwenye Uwanja wa Mkwakwani mjini Tanga, wakati beki wa Coastal Union Bakari Mwamnyeto alipoingia kwenye orodha ya mabeki walioijifunga wenyewe.

Aliisawazishia Mbeya City bao dakika ya 49, wakati huo ikiwa nyuma ya bao 1-0 lililofungwa na Ayou Lyanga na timu hizo zikatoka sare ya bao 1-1.

**6. Omari Salum-(African Lyon vs KMC)**

Januari Mosi mwaka huu, beki wa African Lyon alijifunga bao akiisaidia KMC kushinda mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam, Hassan Kabunda akifunga bao la pili.

**7. Peter Mwangosi-(Mbao FC vs JKT Tanzania)**

Kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, JKT Tanzania iliichapa Mbao FC bao 1-0 Januari 20, mwaka huu.

Bao hilo lililoifanya JKT kushinda ugenini lilifungwa na beki wa Mbao FC, Peter Mwangosi ambaye aliuweka mwenyewe wavuni kwenye harakati za kuokoa.

**8. Rolland Msonjo-(African Lyon vs Azam FC)**

Mechi hii ilichezwa kwenye Uwanja wa Karume Machi Mosi, mwaka huu. Azam ilishinda mabao 3-1. Mabao mawili ya washindi yakifungwa na Obray Chirwa na mwenzake Mudathir Yahaya. La tatu lilifungwa na beki wa African Lyon, Rolland Msonjo dakika ya 89.

**9. Jumanne El Fadhili-(Prisons vs Singida)**

Jumanne El Fadhili ni beki mwandamizi wa Prisons ya Mbeya. Machi 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa Namfua mjini Singida, alijifunga mwenyewe bao lililoipa ushindi Singida United dhidi ya timu yake ya Prisons na kuifanya kutoka uwanjani ikiwa imelala kwa mabao 2-1.


**10. Ally Ally-(KMC vs Yanga)**

Ally alijifunga dakika ya 67 Machi 10, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa likiwa ni la pili na kuipa Yanga ushindi wa mabao 2-1. Kabla hajajifunga timu hizo zilikuwa sare ya kufungana bao 1-1. Mohamed Rashid, straika wa Simba aliyeko kwa mkopo KMC alifunga bao kabla ya Papy Tshishimbi kuisawazishia Yanga.

# Sajili kubwa za kishindo zilizozingua EPL 2018-19




Keita



Seri



Mahrez



Jorginho



Fred

**LONDON,** England

INAWEZEKANA wanatumia fedha kubwa au la, lakini klabu zinakuwa kwenye hatari kubwa wakati wanaposajili wachezaji wapya. Wanaweza kuwa wachezaji wenye majina makubwa, lakini kwa sababu mbalimbali wanajikuta wanakuwa hawapo kwenye kiwango.

Mifano ya hii ni mingi, kuanzia kwa Alvaro Morata na Michy Batshuayi (Chelsea), Alexis Sanchez (Manchester United), Eliaquim Mangala (Manchester City), na wengineo.

Wakati mwingine, sio kwamba mchezaji kiwango chake hushuka ghafla mara moja, lakini mazingira ya klabu yanaweza kutokuwa rafiki kwa mchezaji. Fikiria kesi ya Diego Forlan.

Nyota huyo wa Uruguay hakufanya vizuri wakati akiwa pale Manchester United, lakini alikuwa mnyama kabisa katika klabu za Villarreal na Atletico Madrid baada ya kuondoka Old Trafford.

Dirisha la uhamisho la majira ya baridi la 2018-19 liliona klabu zilivyojitokeza kwa ajili ya kusaka vipaji ili kufanikisha malengo yao. Cristiano Ronaldo (Juventus), Richarlison (Everton), na Alisson Becker (Liverpool) wamekuwa na mafanikio makubwa tangu watue kwenye klabu hizo.

Kwa upande mwingine, wachezaji waliosajiliwa kwa fedha nyingi wameonyesha matunda yao, lakini wengine hola.

Hapa tunaangalia nyota watano ambao pamoja na kusajiliwa kwa fedha nyingi, wamezikatisha tamaa klabu zao...

**5. Jean Micheal Seri (Fulham)**

Raia huyu wa Ivory Coast akiwa anacheza nafasi ya kiungo alionekana kuvuta hisia za klabu nyingi wakati anakipiga pale katika klabu ya Ufaransa, OGC Nice.

Klabu ya FC Barcelona ilitajwa kuwa miongozi mwa timu zilizokuwa zinamwania, huku kiungo wa zamani wa klabu hiyo, Xavi Hernandez, akinukuliwa akisema Seri alikuwa na DNA ya Barca.

Uhamisho haukutokea, na mwaka mmoja baadaye, alijiunga na Fulham kwa pauni milioni 25. Lakini tofauti na matarajio ya wengi, Seri ameshindwa kutamba hadi sasa.

**4. Riyad Mahrez (Man City)**

Inaweza kuonekana kuwa vigumu kumuhukumu winga huyu wa Algeria, kwa sababu yupo katika timu ambayo huduma yake inatolewa na wachezaji wengine watatu (Raheem Sterling, Bernardo Silva, na Leroy Sane).

Hata hivyo, kiwango chake anapopata nafasi ya kucheza sio cha kuvutia, anaonekana wazi kama si yule aliyekuwa akitamba kule Leicester. Mchango wake kwa Leicester wa kutwaa taji la Ligi Kuu England ulimvutia kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.

Klabu ikaingia mfukoni na kuchomoka na pauni milioni 60, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 ameshindwa kufanya lolote. Sterling na Sane wamefanya kazi bora kwa upande wao, kwa kuwa miguu yao inafanya kazi nzuri.

Mahrez alikuwa akionekana kama mmoja wa mawinga bora zaidi duniani, lakini sasa mambo yamekuwa tofauti kabisa.

Licha ya kufunga mabao 11 na kutoa pasi za mwisho saba katika michezo 37 hadi sasa, kiwango chake sio cha kuridhisha.

**3. Jorginho (Chelsea)**

Mchezaji mwingine ambaye hajawahi kuonyesha ubora wake katika msimu wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu ya England. Muitaliano huyo alinunuliwa sambamba na kocha, Maurizio Sarri kutoka Napoli, kwa pauni milioni 57 na kulikuwa na matarajio mengi juu yake, hasa kwamba angeweza kucheza vizuri katika staili ya kocha Sarri.

Lakini kiwango cha Jorginho wa Chelsea ni tofauti kabisa na kile alichokuwa nacho kule Napoli.

**2. Naby Keita (Liverpool)**

Mengi yalitarajiwa kutoka kwa mchezaji huyu wa kimataifa wa Guinea baada ya kuondoka kule Bundesliga katika timu ya RB Leipzig.

Kiungo huyo mwenye ujasiri alikuwa kwenye rada ya Jurgen Klopp na hatimaye akafanikiwa kumsajili Januari mwaka jana kwa pauni milioni 53 na mchezaji akijiunga na timu hiyo majira ya joto.

Haukuwa msimu wa kwanza wa furaha kwenye Ligi Kuu kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24.

Mambo hayajakwenda kama yalivyopangwa, kwa kuwa majeraha na kushuka kiwango limekuwa tatizo kubwa kwake, huku ujio wa Fabinho ukimfanya kukosa kabisa nafasi.

Amecheza mechi 25 katika mashindano yote (14 akianza). Hajafunga bao lolote au kutoa pasi ya mwisho.

**1. Fred (Man United)**

Wakati nyota huyo wa Brazil alipoitosa Manchester City, mashabiki wa United walikuwa wakipiga kelele za furaha baada ya kuwazidi kete katika usajili huo (ikiwa ni mara ya pili baada ya kuwadizi pia kwa Alexis Sanchez).

Fred aliwasili kwa usajili wa pauni milioni 52 kutoka Shakhtar, huku kukiwa na kipengele cha bonasi ya pauni milioni 61.

Ujuzi wake, ujasiri wake, na akili zilikuwa zina maana ya kumtuma kama 'mpishi' wa Paulo Pogba ili aweze kucheza kwa uhuru zaidi pale mbele.

Lakini matokeo yake ameshindwa kabisa kuthibitisha thamani yake, kuanzia akiwa chini ya Jose Mourinho hadi sasa chini ya Ole Gunnar Solskjaer.


Yale matarajio ya mashabiki wa Man United yametoweka kabisa, hajawa na mchango wowote kwa timu hadi sasa.

## NUKUU

"Nimekuwa nikiishi hapa Madrid, kufanya mambo yangu, lakini nimechaji betri zangu. Nipo tayari kuinoa klabu hii kubwa kwa mara nyingine, imekuwa vigumu kutazama kutoka nje. Ninatazama mbele kufanya kazi na wachezaji tena, kushindana tena. Ni mwenye furaha kurejea tena. Ninataka kufanya na kutoa kile kinachotakiwa kuifikisha klabu inapopaswa kuwa. Mambo yatapaswa kubadilika. Nipo hapa kwa sababu rais ameniita," **Zinedine Zidane baada ya kurejea kwa mara nyingine kuinoa Real Madrid.**



"Hii ndiyo sababu ya Juve kuninunua, kuisaidia katika usiku wa maajabu kama huu, ukweli Atleti ni timu ngumu kukabiliana nayo, lakini tupo imara pia na tumethibitisha tunastahili kusonga mbele. Ni mapema mno kuzungumza kuhusu fainali. Haya ni mawazo unayohitaji katika Ligi ya Mabingwa na tupo kwenye njia sahihi." **Cristiano Ronaldo aliiambia Sky Sport Italia baada kutupia hat-trick na kuitoa Atletico Madrid hatua ya 16-bora Ulaya.**



"[Zinedine] Zidane ni Mfaransa, labda anaweza kufanya kitu fulani na [Kylian] Mbappe," **Rais wa Real Madrid, Florentino Perez aliwaambia wanahabari wakati wa utambulisho wa kureja tena kwa kocha huyo, na alipoulizwa ni nani atamchagua kati ya Neymar na Mbappe, Perez alisema: "Wote."**



# Michezo



Kiungo wa Simba, Claotus Chama (kushoto), akishangilia sambamba na John Bocco, baada ya kuifungia timu yake bao la pili dhidi ya AS Vita kwenye Uwanja wa Taifa juzi.

# SIMBA ILIVYOITEKA AFRIKA KIPIGO AS VITA U/TAIFA

**Na Adam Fungamwango**

HISTORIA imeandikwa baada ya Klabu ya Simba ya Tanzania kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya timu ngumu ya AS Vita.

Mechi hiyo kali iliyochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, ilikuwa ya mwisho kwenye Kundi D, Simba ikikamata nafasi ya pili ikiwa na pointi tisa, nyuma ya Al Ahly ya Misri iliyomaliza nafasi ya kwanza kwa kukusanya pointi 10.

Timu za JS Saoura ya Algeria na AS Vita zimetupwa nje ya michuano hiyo.

Hii ni mara ya kwanza kwa Simba kuifunga AS Vita baada ya kucheza nao mara tano.

Mara ya kwanza ilikuwa ni 1978 kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba ikachapwa bao 1-0 jijini Dar es Salaam na kufungwa tena bao 1-0 kwenye mechi ya marudiano nchini DR Congo, zamani ikiitwa Zaire.

Mara ya tatu timu hizo zilikutana kwenye michuano ya Kombe la Kagame mwaka 2012 iliyofanyika nchini na zikatoka sare ya bao 1-1, mara ya nne ilikuwa kwenye mechi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa zilipokutana DR Congo na Simba kuchapwa mabao 5-0.

Hata hivyo, Simba bado haijaifikia rekodi yake iliyoweka mwaka 1974 ilipofanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali na kutolewa na Mehalla El Kubra ya Misri kwa mikwaju ya penalti baada ya kila moja kushinda kwake bao 1-0.

Yafuatayo ni mambo yaliyojitokeza kwenye mechi hiyo ambayo imeiingiza timu hiyo kwenye vitabu vya kumbukumbu...

**1. AS Vita iliingia kwa nguvu moja**

Mechi ilipoanza tu, AS Vita ilianza kwa kasi na lengo lilikuwa ni kupata bao la mapema ambalo lingeichanganya Simba na haikushangaza walipopata bao la mapema, dakika ya 13 tu kupitia kwa Kazadi Kazengu.

**2. Simba walifungwa bao kama la Lipuli**

Kama ulitazama mechi kati ya Simba dhidi ya Lipuli iliyochezwa kwenye Uwanja wa Samora mjini Iringa, halikutofautiana sana na lile la juzi dhidi ya AS Vita.

Mabeki wa Simba wanatatizo la kucheza na refa kwa kunyoosha mikono, huku wakiomba huruma, wakiuacha mpira na wenzao wanawaadhibu kwa njia hiyo.

Kwenye mechi ya Lipuli, mchezaji mmoja alianguka wakanyoosha mikono huku wamesimama, lakini yule yule aliyeanguka alimpasia mfungaji na kuuweka wavuni, ingawa Simba ilishinda mabao 3-1.

Mechi dhidi ya AS Vita, Erasto Nyoni alionekana kuangushwa na straika wa wapinzani wao, mabeki wa Simba badala ya kuuondoa kwanza, wakainua mikono juu, wakiomba huruma ya refa, wakaadhibiwa.

**3. Mabao kufungwa na wasiotarajiwa**

Kwenye mechi hiyo ya kihistoria, mabao ya Simba yalifungwa na wachezaji ambao hawakutarajiwa kabisa na mashabiki.

Mohamed Hussein 'Tshabalala' alifunga bao la kwanza, mchezaji ambaye ni aghalabu sana kufunga bao hata kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania au michuano mingine yoyote ile.

Pamoja na Clatous Chama kuwa mchezaji bora na aliyeiingiza Simba kwenye hatua ya makundi kwa bao lake dhidi ya Nkana FC, lakini hakuna aliyetarajia kuwa angeweza kuwa mkombozi kwa mara nyingine tena.

Ni kwa sababu kwa siku za karibuni Chama ameonekana hayupo kwenye kiwango chake kilichozoeleka, lakini ni yeye ambaye bao lake la dakika za mwishoni lililoipeleka Simba robo fainali kama alivyoiingiza kwenye hatua ya makundi.

**4. Niyonzima aliwavuruga Wakongomani**

Moja kati ya mabadiliko aliyoyafanya kocha wa Simba ni kumtoa Emmanuel Okwi ambaye hakuwa kwenye kiwango chake cha kawaida na kumuingia Haruna Niyonzima.

Mabadiliko hayo kwa kiasi kikubwa ndiyo yaliwavuruga na kuwaumiza kabisa Wakongomani hao. Simba ilikuwa inacheza na viungo watatu, huku AS Vita ikiwa na viungo wanne, hivyo wageni hao walitawala kati.

Lakini baada ya kuingia Niyonzima, akabadilisha kabisa mwenendo wa mchezo na kufanya timu yake itawale kati kwa kiasi kikubwa.

Uwezo wa kuuchezea mpira atakavyo, pasi za haraka zisizotabirika kuwa zitakwenda kwa nani, unyumbulifu wa hali ya juu na ubunifu, uliwafanya viungo wa AS Vita kupoteana kabisa na kuwapa nafasi viungo wa Simba kutamba na kufanikiwa kupata bao la pili dakika ya 90.

**5. Erasto aliituliza beki Simba**

Beki ya Simba ilikuwa kwenye wakati mgumu alipokuwa ameumia Erasto Nyoni na inawezekana kabisa ndiyo ilisababisha Simba kufungwa mabao 5-0 dhidi ya AS Vita na Al Ahly ugenini, lakini kwenye mechi ya Jumamosi alikuwa ndani ya dimba na umuhimu wake ulionekana licha ya kuwa huo ulikuwa mchezo wa kwanza kwake kucheza tangu atoke kwenye chumba cha majeruhi.

Nyoni aliituliza kabisa safu ya ulinzi ya Simba ambayo mara nyingi hukatika na hasa inapokutana na timu zenye mastraika wanyumbulifu na wenye kasi, lakini kwenye mechi hiyo ilitulia, huku akifuta makosa ya wenzake, akicheza kwa ufundi na utulivu wa hali ya juu.

**NAJUA WAJUA**

MANCHESTER City imepoteza kila mechi kati ya nne ilizocheza mechi za michuano ya Ulaya dhidi ya timu kutoka England. Imepoteza mara mbili dhidi ya Chelsea mwaka 1971 na mara mbili dhidi ya Liverpool hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa msimu uliopita. Msimu huu itakutana na Spurs hatua ya robo fainali.

MAKALA

# ZIDANE ANAVYOJUA KUJITENGENEZEA MASIKA YAKE REAL



**MADRID,** Hispania

MOJA ya kosa kubwa ambalo wengi huwa tunalifanya ni pale tunapojisahau na kuamini kuwa furaha zetu hutegemea kitu au mtu.

Yaani bila mtu au kitu fulani ni ngumu kwetu sisi kupata furaha. Hapo ndipo hatua ya kwanza ya maumivu inapoanzia.

Hapo ndipo palipo na chimbuko la maumivu ndani yake. Maisha ni furaha, hiki ndicho tunachotakiwa kukijua.

Tunatakiwa kuishi maisha yenye furaha ndani yetu. Na furaha siku zote hutengenezwa na mtu mwenyewe. Hakuna furaha ambayo mwanadamu yeyote hutengeneza kwa ajili ya mwanadamu mwingine.

Na kama ipo hiyo itakuwa furaha ya muda mfupi na siyo furaha ya muda mrefu. Kipi unakitafuta katika maisha yako? Furaha inayoyeyuka au furaha inayosimama kama mwamba?

Hili ni swali muhimu sana. Swali ambalo huja na mwongozo sahihi wa kupata furaha. Furaha ya dhati hupatikana kwenye mikono ya mhusika mwenyewe.

Ndiyo maana tunashauriwa sana kujifunza kutafuta furaha. Hapa ndipo ambapo tunapokuja kuona namna ambavyo Zinedine Zidane alivyo na uwezo mkubwa wa kujitafutia furaha.

Anapenda kuishi kwenye furaha, anapenda kuishi kwenye sehemu ambayo kuna masika. Masika ambayo yanaweza kumsaidia kwenye kilimo chake.

Anajua kabisa jinsi ya kujitengenezea mazingira ya masika, anajua kabisa kujitengenezea mazingira ya kumpa furaha.

Yaani kwa kifupi anajua kutengeneza furaha kwa mikono yake mwenyewe. Wakati anachaguliwa kuwa kocha wa Real Madrid alifanikiwa sana na timu hii.

Alibeba Ligi ya Mabingwa barani Ulaya mara tatu mfululizo. Alikuwa na kikosi imara sana. Kikosi ambacho kilikuwa na Cristiano Ronaldo.

Mwanadamu ambaye alikuwa anafunga mabao kuanzia 50 ndani ya msimu mmoja. Kwa hiyo wakati yupo Real Madrid alikuwa na uhakika wa timu yake kupata mabao 50 kupitia mtu mmoja tu!

Alikuwa na wapishi mahiri wa mabao, Toni Kroos alikuwa mpishi bora sana. Luka Modric alikuwa mhimili mkubwa sana ndani ya kikosi cha Real Madrid.

Akamtengeneza Casemiro kuwa kiungo bora wa eneo la kuzuia. Sergio Ramos alikuwa beki imara.

Beki ambaye alikuwa anauwezo mkubwa wa kuyalinda mabao na alikuwa na uwezo wa kuyafunga pia hayo.

Unamkumbuka Marcelo? Beki ambaye alikuwa na sifa nyingi sana za kuwa mshambuliaji?

Huyu alikuwapo kwenye kikosi chake na akamfanya kuwa beki ambaye alikuwa anatengeneza nafasi nyingi za mabao yeye pamoja na Dani Carvajal.

Lakini taratibu hali ya dalili ya kiangazi ilianza kuonekana katika klabu ya Real Madrid, Ronaldo aliondoka.

Toni Kroos na Luka Modric wakawa wameshuka kiwango. Vivyo hivyo kwa Dani Carvajal na Marcelo.

Dalili za kupata Real Madrid ambayo ni dhaifu zilianza kuonekana. Ndipo hapo Zinedine Zidane alipoamua kujitoa taratibu na kupumzika kwa muda.

Akaiacha Real Madrid dhaifu, Real Madrid ambayo kwa hivi karibuni imefungwa mechi tano mfululizo katika uwanja wao wa nyumbani zikiwamo mechi mbili dhidi ya Barcelona.

Real Madrid ambayo imetolewa kwenye Ligi ya Mabingwa barani Ulaya na Ajax kwa kufungwa katika uwanja wao nyumbani.

Ni Real Madrid ambayo iko nafasi ya tatu katika Ligi Kuu ya Hispania (La Liga) ikiwa nyuma kwa alama 12 kutoka timu inayoongoza ligi hiyo.

Msimu umekaribia kuisha, Zidane anarudi tena Real Madrid. Anarudi kipindi ambacho watu wengi hawatamhukumu kwa matokeo haya ya mwishoni.

Kitu kizuri kuwa tunaenda kuingia katika dirisha kubwa la usajili, dirisha ambalo litampa nafasi yeye kusajili wachezaji nyota ambao atatembea nao.

Tayari amekuja kipindi ambacho anauwezo wa kujitengenezea masika yake. Kipindi ambacho anauwezo wa kujitengenezea furaha yake mwenyewe.

Kipindi ambacho ana uhakika wa kuingia sokoni kumchukua Mbappe, Neymar, Hazard kwa ajili ya kuendelea kutengeneza Ufalme wake pale Santiago Berbaeu, hebu tusubiri tuone!

**NDANI YA 18**

UNAPOZUNGUMZIA mchezaji mwenye mabao mengi hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, anayepaswa kusimama ni Cristiano Ronaldo kutokana na mabao yake 63, ambapo Lionel Messi anafuata kwa kucheka na nyavu mara 40, Raul (34). Thierry Henry (21), Thomas Muller (21) na Andriy Shevchenko (21).



Nipashe **Spotika**



INAWEZEKANA wanatumia fedha kubwa au la, lakini klabu zinakuwa kwenye hatari kubwa wakati wanaposajili wachezaji wapya. Wanaweza kuwa wachezaji wenye majina makubwa, lakini kwa sababu mbalimbali wanajikuta wanakuwa hawapo kwenye kiwango.

**Uk. 16-17**

# WACHEZAJI 10 BORA LIGI KUU ENGLAND KWA SASA



Van Dijk

**LONDON,** England

MBIO za msimu wa 2018-19 zinaelekea mwisho, huku Manchester City ikiongoza kwa pointi moja zaidi ya Liverpool baada ya kufikisha mechi 30.

Na hii ni kutokana na ukweli kwamba, Liverpool walipoteza pointi moja baada ya kutoka sare na Everton pale Goodison Park katika mechi ya 29 na City haikushindwa kuitumia nafasi hiyo, hivyo wakashinda dhidi ya Bournemouth na Watford. Chini yao kuna ushindani tena mkubwa kwa timu nne zinazowania nafasi mbili za kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo kwa sasa zinashikiliwa na Tottenham na Arsenal. Tottenham ilikuwa pointi 10 mbele ya Arsenal iliyopo nafasi ya nne siku 16 zilizopita, na sasa wamepishana kwa pointi moja tu.

Baada ya kushinda kwa staili ya kuvutia alipopewa mikoba pale Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer alipata kipigo chake cha kwanza kwenye Ligi Kuu kutoka mikononi mwa Unai Emery na Manchester United imeshuka hadi nafasi ya tano. Chelsea wao wamejikuta kwenye wakati mgumu na sasa wanajaribu kupambana kurudi kwenye nne bora.

Hebu tuangalie wachezaji 10 bora zaidi katika ligi hiyo baada ya mechi ya 30...

**10. Granit Xhaka (Arsenal)**

Granit Xhaka pengine ni mchezaji aliyechukiwa sana pale Arsenal pamoja na Mustafi, kutokana na mchezaji huyo wa kimataifa wa Uswisi kutokuwa na kiwango bora katika misimu michache iliyopita. Hata hivyo, kwa sasa tunamuona Granit Xhaka mwenye ujasiri zaidi, mwenye uwezo na hii ni kwa sababu ya Unai Emery.

Ingawa bado anaonyesha hali ya kutofautiana, Xhaka amekuwa mchezaji muhimu kwa Arsenal katika kampeni ya msimu huu, mara nyingi huleta mabadiliko ya ziada akiwa dimbani. Kutua kwa Torreira na Guendouzi kumemfanya kuwa kwenye tishio la kukosa nafasi katika kikosi cha kwanza.

**9. Aaron Wan-Bissaka (Crystal Palace)**

Mchezaji huyu wa kimataifa wa England ni mmoja wa wachezaji wenye miguu inayotikisa dunia kwa sasa. Aaron Wan-Bissaka amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu kwa kikosi cha Crystal Palace kinachofanya vizuri msimu huu, huku akiisaidia kutoka kwenye hatari ya kushuka daraja na sasa wapo nafasi ya 14 kwenye msimamo. Wan-Bissaka kwa umri wake wa miaka 27, ameanza katika michezo 27 kwa Crystal Palace msimu huu, na kukosa mitatu tu kutokana na kuumia.

**8. Alisson Becker (Liverpool)**

Kwa mshangao Alisson Becker ameingia kwenye orodha tena. Becker amekuwa na kiwango kizuri pale Liverpool na mashabiki wanaonekana kumwelewa. Raia huyo wa Brazil mwanzo alifanya makosa mengi, lakini sasa anaonyesha thamani yake.

Allison Becker ameingia katika rekodi ya kuwa golikipa aliyecheza mechi nyingi za Ligi Kuu, (17) bila nyavu zake kutikiswa, akifuatiwa na Ederson (14). Upatina wake na Van Dijk na Matip umeimarisha safu ya ulinzi msimu huu.

**7. Alexandre Lacazette (Arsenal)**

Maneno hayatoshi kuelezea mapenzi waliyonayo mashabiki wa 'Washika Bunduki' hao kwa Alexandre Lacazette. Mfaransa huyo amekuwa akipendwa tangu siku ya kwanza na anazidi kuimarika siku hadi siku.

Ingawa mara zote Lacazette anapenda kucheza sambamba na Aubameyang, lakini uwapo wa mshambuliaji huyo wa Gabon umemfanya yeye kucheza pembeni.

**6. Fernandinho (Man City)**

Ingawa Fernandinho alikosa mechi nyingi za Manchester City kutokana na kuwa majeruhi, haitakuwa sawa kutomuweka kwenye orodha hii. Fernandinho ni mchezaji ambaye Pep anapata wakati mgumu wa kutafuta mrithi wake na utaelewa kwa nini.

Fernandinho ni mchezaji ambaye unaweza usimuone uwanjani, lakini kazi yake ikawa muhimu zaidi kwa timu. Anacheza nafasi ya kiungo mkabaji ambaye pia huweza kusaidia mashambulizi kwa timu.

**5. Paul Pogba (Man United)**

Ole Gunnar Solksjaer amekuwa moto pale Manchester United. Kocha huyo wa muda ameiongoza vizuri zaidi United kwasababu ameijenga kuwa timu ya ushindani.

Mbinu zake zinawafanya wachezaji kucheza kwa uhuru na kujiachia na hilo limemfanya Paul Pogba kuwa na wakati mzuri zaidi. Mshindi huyo wa Kombe la Dunia amefunga mabao saba na kutoa pasi za mwisho tano katika mechi 13 chini ya Ole na anaonekana kuwa kwenye kiwango bora kabisa.

Ingawa Ole alifungwa mechi yake ya kwanza kwenye Ligi Kuu na Arsenal, timu yake ina kitu ambacho wengi wangekihitaji. Pogba, sambamba na Matic na Herrera, wameifanya timu hiyo kuwa kwenye kiwango kizuri.

**4. Sergio Aguero (Man City)**

Hakuna mshambuliaji hata mmoja barani Ulaya anayeweza kushindana na Sergio Aguero kwa sasa.

Aguero anaongoza katika mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora, baada ya kukosekana dimbani kwa kipindi cha mwaka mmoja kutokana na kuwa majeruhi. Kwa mara ya mwisho alichukua Kiatu cha Dhahabu msimu wa 2014-15 wakati Manchester City waliposhinda taji la Ligi Kuu na Sergio alifunga mabao 34. Kwa sasa anaongoza msimamo wa wafungaji baada ya kufunga mabao 18, huku Aubameyang, Kane na Salah wakimfukuza kwa nyuma na mabao yao 17 kila mmoja.

**3. Lukasz Fabianski (West Ham)**

Fabianski ndiye golikipa pekee ambaye timu yake haipo kwenye sita bora kuwapo kwenye orodha hii. Katika umri wake wa miaka 33, amekuwa msaada mkubwa zaidi kwa West Ham kwa kuokoa hatari kadhaa. Licha ya kwamba makipa wengine kama Alisson na Ederson wamekuwa kwenye kiwango bora, lakini Fabianski yupo juu yao.

**2. Virgil Van Dijk (Liverpool)**

Mchezaji wa zamani wa Southampton, amekuwa akiiongoza vizuri zaidi safu ya ulinzi ya Liverpool. Van Dijk unaweza kumtaja kama beki bora msimu huu akiwa chini ya kocha, Jurgen Klopp.

Liverpool imeruhusu kufungwa mabao 17 kwenye Ligi Kuu msimu huu, lakini shukrani zote zinakwenda kwa Van Dijk kutokana na uwezo wake na tayari ameonyesha thamani yake ya pauni milioni 75.


**1. Raheem Sterling (Man City)**

Wakati msimu ukikaribia mwisho, Raheem Sterling ameonyesha uwezo wake mkubwa zaidi katika kufunga. Amekuwa mchezaji mwenye kiwango kisichoshuka katika Klabu ya Manchester City msimu huu. Hakuna beki anayetaka kumkaba mchezaji kama Sterling, ambaye thamani yake inaonekana kuwa juu zaidi siku hadi siku na anaonekana kuwa bomba mbaya chini ya kocha Pep Guardiola.

Katika umri wake wa miaka 23, amefunga mabao 15 kwenye mechi 27 alizoichezea Manchester City Ligi Kuu, akitoa pasi za mwisho tisa.

**USILOLIJUA**

PEP Guardiola amefuzu robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya [akiwa kocha] mara tisa katika misimu yake 10 aliyoshiriki, msimu pekee alioshindwa kufanya hivyo ni 2016-17.





# Vijana waziona, wazitumia fursa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIJANA 85 wa kata sita za Jiji la Mbeya wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali ikiwamo kutengeneza bidhaa mbalimbali ili kujikwamua kiuchumi, kujiajiri na kuepuka utegemezi.

Mafunzo hayo yalitolewa na mashirika ya kiraia ya Shop na The Foundation for Civil Society katika kata za Iyela, Isyesye, Ilemi, Ilomba, Maanga na Ruanda ambapo vijana hao waliunganishwa kwenye vikundi.

Katibu wa Shop, Olais Oleseenga, alisema ili kutekeleza mradi huo walipewa ruzuku ya shilingi milioni 30 kuwapatia elimu vijana wa kata sita jijini hili.

Alisema lengo la mradi huo ni kuhakikisha vijana wanakuwa kiuchumi na kuimarika kwa kufanya ujasiriamali ambao utakuwa na manufaa kwao, vikundi mbalimbali na taifa.

Alisema awali shirika hilo lilitoa elimu kwa vijana juu ya kuzitambua fursa mbalimbali zinazowazunguka ndani ya kata zao na kutambua sera ya vijana ya 2007 na baadaye wakaanza kutoa elimu ya ujasiriamali.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Jiji la Mbeya, Onna Geofrey, alisema kwa sasa vijana wanatakiwa kujiunga kwenye vikundi ili kuweza kunufaika na fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali kupitia mifuko ya vijana.

# Wajasiriamali waonywa kujitwika majukumu yote

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI

ASILIMIA 80 ya biashara zinazoanzishwa sehemu mbalimbali haziendelei kutokana na wamiliki wake kutozingatia misingi ya uendeshaji, ikiwamo kutekeleza majukumu yote wenyewe badala yake kuunda timu ya utatu kushughulikia maeneo muhimu.

Aidha, timu hiyo ya utatu huundwa na wasimamizi wa uzalishaji, watafuta masoko na wasimamizi wa fedha na kwamba ndicho wanachowafundisha wajasiriamali sasa.

Hayo yalisemwa juzi wilayani Mbozi mkoani Songwe na Mwenyekiti wa Taasisi ya Sirolli kutoka nchini Marekani, Dk. Ernest Sirolli, kwenye Mradi wa Uwezeshaji wa Biashara (Sirolli) kwa wajasiriamali wa Wilaya ya Mbozi mkoani humo.

Mradi huo unafadhiliwa na Shirika la Heifer International na kutekelezwa na shirika hilo kwa kushirikiana na Taasisi ya Sirolli, unaotekeleza na taasisi hiyo kwa kushirikiana na Shirika la Heifer International ambalo pia ndilo mtekelezaji.

Alisema ili biashara yoyote iweze kufanikiwa ni lazima iendeshwe kwa kuunda timu ya utatu yaani kuwapo na wasimamizi wa uzalishaji, watafuta masoko na wasimamizi wa fedha na kwamba ndicho wanachowafundisha wajasiriamali wa Mbozi.

Aliongeza kuwa mradi huo ni wa majaribio na unafanyika kwa muda wa miaka miwili kuanzia Oktoba 2017 na unatarajiwa kufikia ukomo Juni 2019 na kwamba unafadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Heifer International.

"Tunatoa ushauri bure na kwa usiri kwa mtu yeyote anayehitaji, mwenye wazo la biashara au anataka kukuza na kuendesha biashara, ni muhimu mjasiriamali kujua mahali soko lilipo, ubora wa bidhaa zinazohitajika na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha," alisema Dk. Sirolli.

Makamu Mwenyekiti wa Shirika la Heifer International Tanzania, Rose Marando, alisema mradi huo ni wa vikundi na unalenga kuimarisha biashara za vikundi hivyo kwa kutoa elimu juu ya uendeshaji wa biashara hizo.

Aliwaeleza wajasiriamali kuwa Heifer International iliamua kufadhili mradi huo baada ya kubaini kuwa wajasiriamali wengi wanakabiliwa na changamoto nyingi kama kukosa saikolojia ya biashara kwa kutojua taratibu za utunzaji wa kumbukumbu na kutenganisha mtaji na faida.

Alisema wakati mwingine wajasiriamali wanajikuta kila kitu kinakuwa kigumu kwao kwa kujikuta wakati mwingine wanachukua mtaji na kuingiza kwenye matumizi ya nyumbani.

"Mara nyingi tumeona mjasiriamali huyo anazalisha bidhaa, anatafuta masoko mwenyewe na anatunza fedha mwenyewe hali ambayo inafika wakati vyote vinakuwa vigumu kwake, sasa tumekuja na kitu kinaitwa 'utatu wa biashara' au business psychology (saikolojia ya biashara au Trinity of management"), alisema Marando.

Alisema kikundi kinaweza kikawa cha marafiki ama wanafamilia ili mradi wanaelewana na kila mtu anatakiwa kufanya kitu anachokifahamu na kwamba mradi huo utasaidia kuondoa fikra za jamii kuwa fedha zao zinachukuliwa na 'chuma ulete.'

Ofisa Uhusiano wa Heifer International Tanzania, Mercy Nyanda, aliwataka wafanyabiashara wa Wilaya ya Mbozi kuutumia vizuri mradi huo kwa maelezo kuwa utawasaidia kuimarisha biashara zao kwa kuhakikisha zinakuwa endelevu.

Alisema mradi huo una madaktari wa biashara ambao watawapatia elimu ya namna ya kuendesha biashara zao kwa faida na kutunza kumbukumbu za biashara hizo.



Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, John Palingo (kulia), akizungumza na baadhi ya wajasiriamali wa wilaya hiyo walionufaika na mradi wa uwezeshaji wa biashara unaotekelezwa na Shirika la Heifer International kwa kushirikiana na Taasisi ya Sirolli. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waziri Mbarawa akerwa usimamizi duni miradi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI wa Maji na Umwagiliaji, Profesa Makame Mbarawa, amekerwa na uzembe wa kutosimamia miradi ya huduma hiyo na kusababisha wananchi wa kata nne za jiji la Mbeya kukosa majisafi, akielekeza lawama kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA).

Profesa Mbarawa alionyesha kukerwa na hali hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa anazungumza na watumishi wa WSSA ikiwa ni sehemu ya ziara yake ya siku tatu mkoani Mbeya kwa ajili ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maji na hali ya upatikanaji wa huduma hiyo.

Kata hizo ni Uyole, Isyesye, Nsalaga na Itezi zilizoko kaskazini mashariki mwa jiji.

Kufuatia hali hiyo, alitoa miezi miwili kwa Mbeya-WSSA kuhakikisha wananchi hao wanasambaziwa huduma hiyo ili kuondoa changamoto zinazowakabili.

"Ndani ya miezi miwili wananchi wa maeneo hayo wapelekewe majisafi, pesa zinapatikana wapi ni kazi ya bodi na si yangu kwa sababu fedha zinazohitajika si zaidi ya milioni 200 na hii bodi imepewa mamlaka ya kufanya kazi hiyo," alisema Prof. Mbalawa.

Alisema serikali kuu inahusika na kutafuta fedha kwa ajili ya miradi mikubwa, lakini kwenye usambazaji zinahusika mamlaka za mikoa.

Vilevile waziri alizitaja sababu mbili za miradi mingi ya maji kushindwa kukamilika kwa wakati ikiwamo usimamizi mbovu wa mamlaka za maji za mikoa pamoja na utendaji mbovu wa mamlaka hizo sehemu nyingi nchini.


Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Mbeya-WSSA, Meneja wa Ufundi wa mamlaka hiyo, Ndele Mengo, alisema wanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa maji kwenye vyanzo hasa kipindi cha kiangazi.

Alisema hali ya upungufu wa maji inasababishwa na uharibifu wa mazingira kwenye vyanzo vya maji na hivyo kiwango cha huduma hiyo kupungua ikilinganishwa na wananchi wanaohitaji.

Alisema kwa sasa wameanza kuchukua hatua mbalimbali ya kulinda vyanzo hivyo ili visiendelee kuharibiwa na kutoa elimu na kuimarisha ulinzi kwenye maeneo hayo. Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Mbeya-WSSA, Dk. Luitico Mwakalukwa, alisema kutokana na uhaba wa maji unaokabili Jiji la Mbeya, kuna maeneo tayari yana miundombinu ya maji lakini wananchi hawapati huduma.

Aliiomba serikali kuu kuisaidia mamlaka hiyo fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji kutoka katika Mto Kiwira ambao unatarajiwa kugharimu zaidi ya Shilingi bilioni 70 na kwamba ndiyo utakaomaliza changamoto hiyo ya maji.

Kwa mujibu wa takwimu za Mbeya-WSSA, mahitaji ya maji Mbeya ni lita milioni 60 kwa siku, lakini uwezo wa kuzalisha kwa sasa ni lita milioni 48 hivyo kuna upungufu wa lita milioni 12.





## Waomba uhuru wa watafiti, safari za nje

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UMOJA wa Jumuiya za Wanataaluma wa Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki vya Umma nchini (Asapuct), umeiomba serikali kuendelea kutoa uhuru kwa wanataaluma kwenye masuala ya utafiti na safari za nje ya nchi.

Rais wa Asapuct, Dk. Eliapenda Mariki, alitoa ombi hilo jijini Dodoma mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya kumuaga Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ali aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Asapuct.

Alisema changamoto ya kuchelewa kushughulikiwa kwa vibali vya safari za nje kwa kiasi kikubwa imeshughulikiwa, lakini vibali vya utafiti bado ni tatizo.

Mariki alisema baadhi ya vyuo vimeanza kulalamika kuhusu vibali hivyo vya utafiti na kuiomba serikali kuendelea kutoa uhuru kwa wanataaluma hao.

Kiongozi huyo pia alikemea vitendo viovu vinavyofanywa na baadhi ya wanataaluma ikiwa ni pamoja na kujihusisha na vitendo vya rushwa ya ngono.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU), Dk. Paul Loisulie, alisema wanataaluma wanashauri kurudishwa kwa muda wa hati za kusafiria uliokuwa ukitolewa zamani kwa watu wanaotaka kusafiri kwenda nchi za Afrika Mashariki.

"Kwa sasa ukipewa hiyo hati, ukirudi ndiyo basi, muda wake umemalizika, huwezi kuitumia tena, kwa hiyo tunawanyima Watanzania fursa ya kuwasiliana na wenzao wa Afrika Mashariki," alisema.

Dk. Loisulie aliongeza kuwa Dk. Bashiru ametoa mchango mkubwa kwenye jumuiya za wanataaluma kwa kuandaa maandiko mbalimbali kwa lengo la kutetea maslahi ya wanataaluma na elimu ya juu nchini.

Akizungumzia suala la vibali vya safari za nje ya nchi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, alisema wizara inatambua mchango wa wanataaluma nchini, ndiyo maana imerahisisha utoaji wa vibali vya kusafiri na kuruhusu kufanya usajili mtandaoni.

"Suala hili limeshughulikiwa na kwa sasa tunatia saini vibali vya wanataaluma kwa wakati, hadi usiku wa manane tunafanya kazi ya kupitia vibali, wakati mwingine mtu akiomba tunamwambia kabisa tangulia 'airport' (uwanja wa ndege) utakutana nacho," alisema.

Akiwaaga wanataaluma hao, Dk. Bashiru alisema atafanya kila linalowezekana kuhakikisha kunakuwa na mazingira mazuri ya kufundisha na kujifunza.

Kiongozi huyo wa CCM pia alieleza kukerwa na wanataaluma wa vyuo vikuu wenye njaa ya madaraka kwa kuwa wamekuwa wakiibua "vita kubwa ya kusaka uongozi" kati yao na wakuu wa idara kwenye vyuo vikuu nchini.

Alisema kwenye mchakato huo wa uongozi, huibuka vikundi vya watu ambao hupanga safu kama chama cha siasa bila kuzingatia sifa, uadilifu na weledi wa kitaaluma.

"Nilipokuwa UDSM (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam). Michakato miwili ilifutwa kwa kuwa ilikuwa kichefuchefu. Kumekuwa na tabia ya kuibuka vikundi vya watu kupanga safu kama vyama vya siasa," alisema.

# Bunge lataka miradi yenye hadhi Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeutaka uongozi wa Jiji la Dodoma kuhakikisha unasimamia ujenzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwenye maeneo mbalimbali, ili iendane na hadhi ya makao makuu ya nchi.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki baada ya kutembelea na kukagua ujenzi wa kituo cha mabasi yaendayo mikoani, ujenzi wa soko na barabara mbalimbali jijini.

Alisema kamati imeridhishwa na kasi ya ujenzi wa miundombinu hiyo na kusisitiza kuwa ujenzi wake ufanyike kwa viwango vinavyotakiwa kulingana na hadhi ya jiji hilo.

Kaboyoka pia aliagiza kuwapo kwa usafi wa mazingira kwa kuwahimiza wananchi na kutunga sheria ndogo zitakazotoza faini kwa wasiosafisha maeneo yao.

Akitoa maelezo ya miradi hiyo, Mkurugenzi wa Jiji hilo, Godwin Kunambi, alisema kwa miradi ya barabara ndani ya jiji (barabara mchepuko) unagharimu zaidi ya Sh. bilioni 18 na fedha zilizolipwa hadi sasa ni zaidi ya Sh. bilioni nne, zikitarajiwa kukamilika Septemba mwaka huu.

Alisema kituo cha mabasi kinachojengwa kitafanya kazi saa 24 na kitakuwa cha aina yake, huku akibainisha kuwa Jiji la Dodoma nalo linatarajia kuwa na mabasi yake.

"Na mabasi hayo yatafanya kazi ya kubeba abiria watakaoshuka kutoka stesheni au uwanja wa ndege na kupelekwa kituo hicho cha mabasi, lengo letu ni kumuunganisha mtu na usafiri wa anga, reli na barabara na ndiyo makao makuu inatakiwa iwe," alisema.

Kunambi alisema ujenzi wa miradi hiyo umewanufaisha wananchi 850 kupitia ajira.

"Miradi yote ya Benki ya Dunia (kituo cha mabasi, soko na barabara) inagharimu Sh. bilioni 77.7, imefanya mzunguko wa fedha Dodoma kuwa mkubwa, tunataka Jiji la Dodoma lifanane na majiji mengine duniani," alisema.




Diwani wa Kata ya Mwangata katika Manispaa ya Iringa, Edward Chengula, akiongea na wamiliki wa nyumba wa kata hiyo, kuhusu maendeleo na changamoto jana. **PICHA: FRODAY SIMBAYA**

# Wabuni mbinu mpya ya kuwaibia wakulima

**Na Elisante John,** SINGIDA

BAADA ya serikali kupiga marufuku ujazo wa lumbesa katika ununuzi wa mazao kutoka kwa wakulima, baadhi ya wafanyabiashara wamehamishia biashara zao mashambani.

Badala ya kununua vitunguu kwenye Soko la Kimataifa la Misuna lililoko Manispaa ya Singida, wafanyabiashara hao sasa wanawafuata wakulima mashambani na kupima vitunguu kwa kutumia magunia yenye ujazo mkubwa.

Wafanyabiashara hao kutoka ndani na nje ya nchi, wanadaiwa kuwanyonya wakulima kupitia magunia maarufu kwa jina la Tshishimbi, ambayo zimepigwa marufuku na uongozi wa halmashauri kutokana na kuwa na ujazo wa zaidi ya Kg 100.

Kutokana na changamoto hiyo, wakulima wameiomba serikali iwafuatilie wafanyabiashara hao vijijini ili wakulima wanufaike na mazao yao.

Mwenyekiti wa Soko la Misuna, Abdalarahaman Mbogo, alisema wafanyabiashara hao baada ya kudhibitiwa, walichukua magunia hayo na kwenda nayo vijijini ambako wamekuwa wakiyatumia kuwaibia wakulima. "Tunaomba serikali ya mkoa kushirikiana na wenzao wa vijijini na mikoa mingine inayolima zao hili kupiga vita magunia hayo ya nyavu yanayobeba vitunguu zaidi ya Kg 100," alisema.

"Pia, kuna ujanja wa kutumia ndoo kubwa zilizotanuliwa kwa lengo la kumnyonya mkulima kule kule vijijini. Mbaya zaidi, wanapopima kwa ndoo, inabidi mpime ndoo sita ndipo eti wanahesabu gunia moja, jambo hili siyo sawa, wanawanyonya wakulima."

Akizungumzia suala hilo, Mkuu wa Wilaya ya Singida, Paskas Muragili, alikemea matumizi ya vipimo hivyo katika ununuzi wa vitunguu na mazao mengine ya wakulima na kuagiza viongozi wote kushirikiana kuwadhibiti wahusika. Alisema serikali itaendelea na jitihada ya kulinda mazao ya wakulima ili wasiendelee kunyonywa.



## HABARI ZANZIBAR



Meneja Uendeshaji wa Benki ya Exim, Doreen Mcharo (katikati), akizungumza na baadhi ya wateja wa benki hiyo, wakati wa tafrija ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na benki hiyo kwa ajili ya wateja wake wa Jiji la Tanga iliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rais ashangaa kupuuzwa, kutoheshimiwa sheria

**Na Rahma Suleiman,**

ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameonya ya kuwa licha ya kuwapo kwa sheria tisa zinazohusiana na matumizi bora na endelevu ya ardhi, bado watu hawaziheshimu wala kuzifuata.

Akizungumza wakati akifungua semina kuhusu masuala ya ardhi na mali zisizorejesheka iliyofanyika mjini Unguja, alisema lengo la kuhakikisha ardhi inatumika vyema limeifanya serikali kutunga sheria tisa kuhusiana na matumizi bora na endelevu ya rasilimali hiyo.

Alizitaja baadhi ya sheria hizo kuwa ni ya Matumizi ya Ardhi Na. 12 ya Mwaka 1992, Sheria ya Uhaulishaji wa Ardhi Na. 8 ya Mwaka 1994 na Sheria ya Mahakama ya Ardhi Na. 7 ya Mwaka 1994, ambayo ndiyo inayohusiana na uanzishwaji wa mahakama hiyo.

Dk. Shein alisema katika ziara yake aliyoifanya katika wilaya zote za Unguja na Pemba mwezi uliopita amefahamu mengi kuhusiana na kadhia ya kuvunjwa kwa sheria mbalimbali zinazohusiana na matumizi bora ya ardhi.

Alieleza kuwa kwa bahati mbaya wavunjaji wa sheria hizo ni viongozi na watendaji wa serikali na matukio mengine yanayofanywa na wananchi wa kawaida.

"Taarifa za wilaya zilizowasilishwa kwangu zote zimethibitisha kuendelea kuibuka kwa migogoro mipya ya ardhi katika wilaya iko ya uvamizi wa maeneo ya serikali, mingine ni baina ya wananchi na wawekezaji," alisema Dk. Shein.

Aidha, alieleza kuwa jambo jingine ni kuwapo kwa uharibifu mkubwa wa mazingira katika maeneo yanayochimbwa mchanga aliyoyatembelea ikiwa ni pamoja na kuwapo kwa upungufu wa mchanga wenyewe.

Alieleza kuwa katika maeneo aliyoyatembelea katika ziara yake hiyo yakiwamo Donge Chechele, Pangatupu na Kiombamvua kwa Unguja na Finya (Selem) na Shumba Viamboni kwa upande wa Pemba, amejionea hali halisi ya mchanga na kusisitiza kuwa ni mali ya serikali hivyo ni rasilimali ya wote.

Unguja mchanga umepungua kwa kiasi kikubwa tena haupo isipokuwa kuna maeneo sita bado upo, lakini ni maeneo ya kilimo ambayo wananchi wanalima mazao mbali mbali ya chakula, hivyo kunatakiwa maamuzi ya kuendelea na kilimo au kuchimbwe mchanga ambao utachimbwa kwa wastani wa mwaka na nusu, alisema.

Alieleza kuwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na.3 ya Mwaka 2015, pamoja na kanuni zake inafahamisha kwamba mchimbaji mchanga anatakiwa apate kibali, achimbe kwa kuzingatia kima maalum na aingie mkataba wa kurejesha eneo katika hali ya kawaida kama kupanda miti baada ya kumaliziza uchimbaji.

Dk. Shein alieleza kuwa utekelezaji wa sheria hiyo umekosa usimamizi na matokeo yake maeneo mengi yaliokwisha kuchimbwa mchanga yamebaki kuwa majangwa na miti iliyopandwa haikustawi kama ilivyokusudiwa.

Alieleza kuwa takwimu zinaonyesha kwamba yapo magari 750 Unguja na 165 Pemba yanayobeba mchanga na kwamba ni nyingi mno kwa shughuli hiyo na kati ya gari hizo zipo zenye uwezo wa kuchukua hadi tani 30, ambazo nazo kwa kipindi kirefu zimekuwa zikichangia uharibifu wa miundombinu ya barabara.

Dk. Shein alisisitiza haja ya kufanywa kwa utafiti kama anavyosisitiza mara kwa mara katika uongozi wake kwa lengo la kukabiliana na changamoto zilizopo katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Alieleza kuwa kwa kutumia tafiti ndipo itawezekana kuwapo kwa mipango imara ya matumizi ya rasilimali zilizopo sambamba na kuwa na mipango na njia mbadala za kutumia pale inapolazimika kufanya hivyo.

Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati, Salama Aboud Talib, alisema kuwa semina hiyo itasaidia kujua hali halisi iliyopo kuhusu ardhi na mali zisizorejesheka Zanzibar.

# Wadau kuhimiza mabinti kupata chanjo ya saratani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIKA jitihada za kupambana na maradhi yasiyoambukiza kama kansa, Jumuiya ya Magonjwa Yasiyoambukiza Zanzibar, inaendesha mradi wa kutoa elimu kwa wanafunzi wa kike kwenye sekondari na wasichana kuwahamasisha umuhimu wa kupata chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi.

Akiutangaza mradi huo mbele ya waandishi wa habari jana, Mratibu wa Jumuiya hiyo, Haji Khamis, alisema wanatoa elimu kwa wanafunzi hao kuhusu umuhimu wa kushiriki chanjo ya kinga ya saratani ya mlango wa kizazi.

Alisema mradi huo unalenga kuwafikia wanafunzi wa kike 2,000 wenye umri wa miaka 14 kutoka shule mbalimbali za mkoa wa Mjini Magharibi kisiwani Unguja.

Kaimu Meneja wa Kitengo cha Maradhi Yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Omar Abdallah, alisema ushirikiano wa pamoja unahitajika katika kukabiliana na maradhi hayo ili kupunguza idadi ya vifo vinavyotokana na magonjwa yasiyoambukiza.

Aidha, alisema kuwa katika utafiti mbalimbali uliofanywa miaka mitatu iliyopita tatizo la kuongezeka kwa wagonjwa wanaougua maradhi yasiyoambukizwa ni kubwa huku jamii yenyewe ikiwa haijayapa kipaumbele magonjwa hayo.

Alisema wananchi wanaugua kwa wingi maradhi ya shinikizo la damu, kisukari, saratani, figo pamoja na kiharusi kutokana na wananchi kutumia vyakula vyenye mafuta mengi pia vyakula vile vinavyouzwa katika 'super market,' kuacha kufanya mazoezi na kutokula matunda kwa wingi.

Alisema taarifa ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya mwaka jana asilimia 71 ya vifo vinavyotokea duniani vinatokana na maradhi yasiyoambukiza na vingi vinatokea katika umri wa miaka 30 hadi 69 na mataifa ya kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwamo Zanzibar zinaathirika zaidi.

Aidha, alivitaja vichocheo vikubwa vinavyosababisha maradhi yasiyoambukiza kwa Zanzibar kuwa ni mlo usiokamili, kutokufanya mazoezi, utumiaji wa vyakula vyenye chumvi na mafuta kwa wingi.

Omar aliwasisitiza wananchi kujenga utamaduni wa kufanya mazoezi na kutumia matunda kwa wingi kwa kuwa imebainika baadhi ya watu hawajui umuhimu wa matunda katika kupambana na maradhi yasiyoambukiza.

# Udhalilishaji kijinsia bado tishio visiwani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wazee, Wanawake na Watoto, Mwanajuma Majid Abdallah, ametaja udhalilishaji wa kijinsia kuwa ni tatizo kubwa Zanzibar.

Aidha, amesema wanawake na watoto wa Zanzibar wanaendelea kufanyiwa vitendo hivyo licha ya juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na serikali pamoja na wadau wa maendeleo ikiwamo kutoa elimu kwa jamii, lakini vitendo hivyo vinaendelea kuripotiwa kila siku.

Aliyasema hayo katika mkutano na wanahabari ofisini kwake Mwanakwerekwe na kuongeza kuwa vitendo hivyo vimekuwa vikiongezeka kila uchao ikiwamo kubuni njia mpya ya kufanya vitendo hivyo viovu.

Aliitaka jamii kurejesha malezi ya pamoja ya kulinda watoto wao na kuacha muhali wa kutoripoti vitendo hivyo katika vyombo vya sheria badala ya kutumia mitandao ya kijamii.

Aidha, alisema baadhi ya wazazi hawashughulikii suala la kuwaangalia watoto wao bali jukumu hilo huachiwa watumishi wa ndani pekee jambo ambalo ni hatari katika maisha ya sasa yaliyojaa maovu dhidi ya watoto wa kike na wakiume.

"Baadhi ya familia zinaona jukumu la kulea mtoto ni la mfanyakazi pekee, utakuta mzazi wala hashughuliki na mtoto wake, hajui muda wa kwenda wala wa kurudi shule hii ni hatari sana," alionya.

Mkurugenzi wa Sera, Mipango na Utafiti wa wizara hiyo, Mhaza Gharibu Juma, aliwataka wanahabari kufanya uchunguzi juu ya udhalilishaji wa kijinsia ili kuona ni kwa namna gani Zanzibar inapiga hatua katika kukabiliana na vitendo hivyo.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 18 March**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 19 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 20 March**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 21 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 22 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 23 March**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Iljimae
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Be my baby
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 17 March**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Series rpt: Iljimae
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 18 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Kesho Leo
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 19 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum: Uongozi
21:30 Kipindi Maalum: Serengeti boys Uturuki
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 20 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Kesho Leo rpt
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 21 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Elininyo
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Elininyo
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Kipindi Maalum rpt: Uongozi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Riziki
09:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 22 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: Tanesco
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi rpt
13:45 Kipindi Maalum: Serengeti boys Uturuki rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Kipindi Maalum: Serengeti boys Uturuki rpt
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Shamba shape up
19:00 Uchumi na biashara
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 23 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Elininyo
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 24 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Hard price
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Hard price 2
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)





eastafrica RADIO
05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise
88.1FM DAR ES SALAAM


## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

## HABARI KIMATAIFA

## Watu 24 wafariki kwa kimbunga Zimbabwe

**HARARE, Zimbabwe**

WATU 24 wamepoteza maisha mashariki mwa Zimbabwe, baada ya kukumbwa na kimbunga kiitwacho Idai kilichoambatana na mvua kubwa.

Kimbunga hicho tayari kimesababisha vifo zaidi ya 100 katika nchi za Msumbiji na Malawi.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Habari ya Zimbabwe ilieleza kuwa, idadi ya watu waliopotea kutokana na kimbunga hicho imefikia 40 wakiwamo wanafunzi wawili.

Ilieleza kuwa watu takribani 24 wamefariki kusini-mashariki mwa Zimbabwe, ambapo nyumba na madaraja yamesombwa na dhoruba.

Kimbunga Idai ambacho kilisababisha mafuriko na uharibifu kwenye maeneo kadhaa nchini Msumbiji na Malawi kilipiga nchini Zimbabwe siku ya Ijumaa na kusababisha umeme kukatika na mawasiliano mengine.

Wakati huo huo, Mbunge wa Mashariki mwa Wilaya ya Chimanimani, Joshua Sacco, alieleza kuwa kimbunga hicho kimesababisha uharibifu na kwamba imekumbusha kimbunga Eline kilichotokea Februari 2000, ambacho kiliharibu maeneo ya kusini mwa Zimbabwe.

Sacco alisema idadi ya vifo ilitarajiwa kuongezeka, wakati maofisa wakiendelea kutathmini hali ya tukio.

Eneo la Chimanimani linalopakana na Msumbiji limekuwa likiathiriwa vibaya na dhoruba linalosababisha mafuriko pamoja na kuharibu mazao.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa waokoaji wanajaribu kulifikia eneo lililoathirika zaidi la Chimanimani karibu na mpaka wa Msumbiji, hata hivyo zoezi hilo limekwama kutokana na madaraja kusombwa na maji.

*VOA*

**Kimbunga Idai ambacho kilisababisha mafuriko na uharibifu kwenye maeneo kadhaa nchini Msumbiji na Malawi kilipiga nchini Zimbabwe siku ya Ijumaa na kusababisha umeme kukatika na mawasiliano mengine.**

# Wafiwa ajali ndege Ethiopia kupewa majivu wazike

**ADDIS ABABA, Ethiopia**

FAMILIA zilizopoteza ndugu kwenye ajali ya ndege ya Shirika la Ethiopia zimeanza kukabidhiwa majivu ili wafanye maziko kama ishara ya kuwaenzi ndugu zao waliofariki.

Ndege ya Shirika la Ethiopia Boeing chapa 737 Max 8 ilianguka Jumapili iliyopita dakika sita baada ya kuruka kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Bole uliopo mjini Addis Ababa kuelekea Nairobi na kuua watu wote waliokuwamo.

Jana, maofisa wameanza kutoa vifurushi vya majivu yaliyokusanywa kutoka eneo la ajali kwa familia za abiria 157 pamoja na wafanyakazi wa ndege kwa sababu shughuli ya utambuzi wa mabaki ya miili inaweza kuchukua muda mrefu.

Uchunguzi wa vinasaba umeanzishwa kwa lengo la kutambua mabaki ya miili iliyopatikana, lakini wataalamu wamesema unaweza kuchukua muda wa miezi sita.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa familia za waathirika wa kisa hicho ambao ni kutoka mataifa 35 zinapatiwa kiasi cha kilo mbili za majivu ili waweze kuzika kama ishara ya kuwakumbuka ndugu zao.

Ibada ya kuwaombea walipoteza maisha ilifanyika jana mjini Addis Ababa.

*DW*



Waombolezaji wakiweka mashada ya maua ikiwa ni ishara ya kuwakumbuka watu waliouawa kwenye shambulio la kujitoa mhanga kwenye msikiti wa Al Noor na Linwood nchini New Zealand. **PICHA: ALLIANCE**

## New Zealand yaanza kutoa miili ya waliofariki

**WELLINGTON, New Zealand**

MAMLAKA za New Zealand zinatarajia kuanza kukabidhi miili ya watu waliokufa kwenye shambulio la misikiti miwili nchini humo, baada ya jana zoezi la kutoa miili 50 kuanza.

Hatua hiyo itazipa nafasi familia kuanza kuwazika wapendwa wao waliofariki katika shambuli hilo. Wachunguzi wa vifo wamesema wanatarajia kutoa angalau mwili mmoja.

Kulingana na taarifa iliyotolewa na kusambazwa kwa familia za waathirika hao, watu waliokufa ni wa kati ya umri wa miaka 3-77.

Wakati huo huo, mshukiwa wa shambulio hilo, Brenton Harrison, amefikishwa mahakamani nchini New Zealand kujibu tuhuma za mauaji.

Harrison akiwa amefungwa pingu alisimama katika Mahakama ya Wilaya ya Christchurch na baadaye kurejeshwa rumande bila kujibu lolote.

Jeshi la Polisi limesema mshukiwa huyo atarudishwa tena mahakamani Aprili 5, mwaka huu na mashtaka dhidi yake yanaweza kuongezeka.

Shambulio la Christchurch ambalo Waziri Mkuu wa New Zealand ameliitaja kuwa la kigaidi, ndiyo shambulio baya katika historia ya nchi hiyo na limeongeza hofu ya usalama nchini humo.

Ahmed Al-Mahmoud aliyenusurika katika shambulio hilo baada ya kuvunja kioo cha dirisha na kukimbia, akisimulia namna tukio hilo lilivyotokea alisema mshambuliaji aliingia msikitini wakati walipokuwa katikati ya swala.

"Aliingia na kuanza kushambulia kila mtu aliyekuwamo ndani, kila mahali," alisema Al-Mahmoud.

Waombolezaji nchini humo wamewasha mishumaa na kuweka maua katika eneo la kumbukumbu lililowekwa mjini Christchurch. Baadhi ya waombolezaji wameonekana wakiwafariji jirani zao na wengine wakisimama kimya eneo la karibu na misikiti iliyoshambuliwa.

Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Jacinda Ardern, aliungana na jamii ya Waislamu katika kituo cha wakimbizi mjini Christchurch akisema atahakikisha uhuru wa kuabudu nchini New Zealand unakuwapo.

"Ninatoa ujumbe wa upendo na mshikamano kwa niaba ya New Zealand kwenu nyote," alisema Waziri Mkuu Ardern.

Aidha, aliahidi kufanya marekebisho ya sheria ya umiliki wa silaha akisema mshukiwa Tarrant alikuwa na kibali cha kumiliki silaha na alitumia silaha tano.

"Ninaweza kuwaeleza jambo moja, sheria zetu za umiliki wa silaha zitabadilika," Ardern aliwaeleza waandishi wa habari.

Waathirika wengi wa tukio hilo ni wakimbizi na wahamiaji kutoka nchi za Pakistan, India, Malaysia, Indonesia, Uturuki, Somalia na Afghanistan.

Miaka ya nyuma New Zealand iliwahi kujaribu kudhibiti sheria za umiliki wa silaha, na kwa mujibu wa takwimu nchini humo kunakadiriwa kuwapo na silaha milioni 1.5 katika taifa lenye wakazi milioni tano.

Hata hivyo, New Zealand ina kiwango kidogo cha machafuko ya silaha.

Tarrant ambaye ni mzaliwa wa Australia aliishi kwenye kisiwa cha kusini cha New Zealand na alikuwa ni mwanachama wa klabu ya bunduki ya Bruce, kulingana na ripoti za vyombo vya habari ambavyo vilinukuu wanachama wa klabu hiyo, walisema alikuwa akifanya mazoezi ya kulenga shabaha.

*DW*

# HABARI PICHANI



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akipokea tuzo ya heshima kwa ajili ya Rais John Magufuli kutoka kwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, iliyotolewa na Taasisi ya Dk. Reginald Mengi PWD Foundation, wakati wa hafla ya chakula cha mchana na watu wenye ulemavu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA ZOTE: HALIMA KAMBI**




Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, akitoa tuzo ya mafanikio katika ujuzi wa kipekee kwa wanawake kwa Wakonta Kakunda, iliyoandaliwa na taasisi hiyo.



Mbunge wa Vunjo, James Mbatia, akimkabidhi tuzo ya mafanikio katika siasa kwa upande wa wanawake, Mbunge wa Viti Maalum, Amina Mollel.



Baadhi ya watu wenye ulemavu waliohudhuria hafla hiyo.



Mama akimlisha mwanawe chakula.



Baadhi ya washiriki wakipata chakula.

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**WAFANYAKAZI WA HOTELINI**, Wanatakiwa wafanyakazi wa Usafi, Wahudumu, Wapishi na Meneja. Bagamoyo mjini, wawe na vyeti na uwezo wa kuongea Kingereza. Kwa Mawasiliano piga namba: 023-2440004/0657 233970/0768 296667


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**FAIR DEAL AUTO PVT LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya PIKIPIKI aina BAJAJI yenye namba za usajili **MC 263 AST** Chassis **MD2A21BZ8FWA51202,** Engine Namba **PFZWFA35687.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DOM/TR/RB/108/2019.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**FAIR DEAL AUTO PVT LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **BAJAJ BOXER** yenye namba za usajili **MC 290 BTS.** Chassis namba **MD2A21BY5HWE91100.** Engine namba. PFZWHE63179.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DOM/TR/RB/441/2019.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No…18.. Of 2019**
**In the matter of the Estate of the late JEROME JUMA NAMNYAMBE of Hazina within Dodoma City**

**AND**

**In the matter of the Application for letters of Administration by JOSEPH JEROME**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the… 2… Day of…. 4….. 2019.

Dated at Dododma this …… day of ……… 2019

## KUPOTEA KWA VYETI



**CHARLES CHRISTIAN PONERA** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha Kidato cha nne chenye **index namba S.0485/0078** katika sekondari ya MAJENGO Mwaka 2000 na Cheti cha shule ya sekondari SONGEA GIRLS chenye index namba **P.0219/0049** kilichotolewa mwaka 2001, na Driving Licence yenye no. 4000353687.

**Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi.**
**Taarifa polisi:**
**CHA/BI/20/VOL/COX/290**

115121302

**FORM II**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo: MJINI TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi No. 32/2019**

**Ombi la LUCY JOSEPH TEMBA kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu JOSEPH JACOB TEMBA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 27/03/2019. kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 11/03/2019

21512202

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**HOSEA L. MUHUMHA** anatangaza kupotelewa na kadi ya GARI aina ya TATA yenye namba za usajili **T 597 CBB.** Chassis **MAT366534CBR1162** Engine Namba **497TCXY815472.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **DOM/TR/RB/216/2019.**

115121602


KWA MATANGAZO

MADOGO MADOGO

TUPIGIE

0767 223311

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# LIVERPOOL

## HAITAFANYA FUJO SOKONI – KLOPP

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema haitawezekana kwa 'Wekundu' hao kutumia kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya usajili majira ya joto.

Kikosi cha Klopp, Liverpool kipo katika vita ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kutumia mpunga wa haja kuwanunua Alisson, Fabinho, Naby Keita na Xherdan Shaqiri msimu uliopita.

Kabla ya mechi ya jana Liverpool ilikuwa pointi moja nyuma dhidi ya Manchester City iliyokuwa kileleni, wakati pia ikitarajiwa kuwa na shughuli ngumu kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Porto.

Na kocha huyo raia wa Ujerumani, Klopp anataka kuitengeneza timu hiyo kuwa ya ushindani wa makombe kuliko kuendelea kuwekeza zaidi.

"Sitaki kuzungumza hakika nini tutakachokifanya, lakini sidhani hii ni timu ambayo tutakwenda kutumia kiasi kikubwa sokoni ama vinginevyo," Klopp alisema.

"Kitu cha muhimu cha kufanya ni kulileta pamoja kundi hili la wachezaji, kujaribu kuwaendeleza pamoja na kisha kukaa pamoja kwa muda. Na hilo pengine ni tatizo kubwa la Liverpool kwa muongo uliopita.

"Wakati walipokuwa na timu nzuri baada ya msimu walikwenda duniani kote. Kwa uhakika hilo halitatokea mwaka huu."

## ZIDANE AMEANZA KULIPA - CEBALLOS

**MADRID, Hispania**

**Zinedine Zidane ameanza kumaliza baadhi ya kero za kukosolewa kulikokuwa kumetanda Real Madrid, kwa mujibu wa kiungo Dani Ceballos.**

**Madrid iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Celta Vigo, katika mechi ya kwanza Zidane kukiongoza kikosi hicho kama kocha mkuu mwishoni mwa wiki akibeba mikoba ya Santiago Solari, wakati Isco na Gareth Bale wakifunga mabao hayo katika kipindi cha pili.**

**Ceballos alichezeshwa akitokea benchi kuchukua nafasi ya Isco baada ya dakika 62 ya kufunga bao la kwanza na kudai uamuzi wa kumuondoa Solari umeonekana mara moja.**

**"Mabadiliko ya kocha yanaonekana kufanya kazi," alisema. "Timu imekuwa chanya zaidi leo. Kitu cha muhimu zaidi kilikuwa pointi tatu.**

**"Zaidi ya yote, tutakachotakiwa kukifanya sasa ni kukamilisha malengo yetu, ambayo ni kumaliza nafasi ya juu katika msimamo kadri tuwezavyo."**

**Bale mara nyingi alikuwa akitokea benchi chini ya Zidane kuelekea mwishoni mwa msimu uliopita, lakini Jumamosi aliiongoza vema safu ya ushambuliaji kabla ya kuiwezesha timu hiyo kuvuna pointi zote tatu.**

**"Wao ni wachezaji wawili muhimu kwetu. Wanachokifanya ni muhimu kwetu, lakini kuna wachezaji wengine 25," Ceballos alisema.**



# Arsenal yarudi kwa Overmars

**LONDON, England**

MKURUGENZI wa Michezo wa Ajax, Marc Overmars, amerejea katika orodha ya wanaopewa nafasi ya kuwa mkurugenzi wa ufundi wa Arsenal.

Gazeti la The Mirror limeeleza kuwa Mholanzi huyo amekuwa akihusishwa sana na kupewa jukumu hilo kufuatia kuondoka Mkuu wa Idara ya Uajiri Arsenal, Sven Mislintat.

'Gunners' ilitoa kipaumbele kwa Mkurugenzi wa zamani wa Michezo wa Roma, Monchi, lakini kuanzia hapo amekubali kurudi Sevilla.

Kwa sasa Overmars ndiye chaguo la kwanza kuchukua nafasi hiyo, kama atakuwa tayari kuondoka klabu yake ya Ajax.

Hata hivyo, inaonekana itakuwa vigumu kwa Overmars kuondoka kutokana na Ajax kutaka kuendelea kumbakisha nyota huyo wa zamani wa Arsenal mwenye umri wa miaka 45.





# BECKHAM
## AWAOTA MESSI, CR7 MIAMI

**MIAMI, Marekani**

David Beckham bado hajaweka kando suala la kumnasa Lionel Messi ama Cristiano Ronaldo katika klabu yake ya Inter Miami, lakini akakiri ndoto za kufikia mapinduzi hayo ya ajabu ni uwezekano.

Nyota huyo wa zamani wa LA Galaxy, Beckham anajiandaa kuiwezesha klabu yake mpya ya Miami kushiriki Ligi Kuu ya Marekani [Major League Soccer] msimu ujao, wakati huu kukiwa na tetesi za kusajili majina makubwa.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Manchester United, Real Madrid na England, ambaye pia aliichezea AC Milan na Paris Saint-Germain, amekuwa akihusishwa na nyota hao wawili wakubwa duniani, lakini amekataa kuwapo na nafasi ya kumng'oa Messi kwa sasa kutoka Barcelona ama kuishawishi Juventus kuachana na Ronaldo.

"Kila mtu ana orodha yake anayoitaka - kila mtu anafanya! Lakini kama unatazama katika njia Leo na Cristiano bado wanacheza, kwa nini unaweza kufikiria ni hatua ya baadaye mwishoni mwa wasifu wao kisoka, sioni mwisho wao kwa sasa," aliwaambia waandishi wa habari.

"Wanacheza kwa kiwango cha juu ni vigumu kuwaona wakiondoka katika klabu zao walizopo. Lakini tutaona. Huwezi kujua nini kitatokea katika soka."

Beckham alibainisha kuwa ametafuta ushauri kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa zamani wa United, David Gill, miongoni mwa wengine, kama jaribio la Inter Miami kukusanya kikosi chao cha kuanzisha.

## Ramsey atakiwa kuiga kwa Bale

**Cardiff, Wales**

KOCHA Mkuu wa Wales, Ryan Giggs, anatarajia kumuona Aaron Ramsey akimuiga Gareth Bale na kufikia kiwango cha juu, wakati huu akijiandaa kutua Juventus mwishoni mwa msimu.

Ramsey anajiandaa kuhitimisha miaka yake 11 ya kuitumikia Arsenal na kuhamia kwa mabingwa hao wa Serie A, wakati mkataba wake utakapomalizika Juni mwaka huu.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 28, amekuwa akipewa nafasi mara kwa mara katika klabu na timu yake ya taifa, na bado Giggs anatumai Ramsey atakwenda kuwa na wakati mzuri Italia.

"Umeona kinachoendelea nje kwa Gareth. Itakuwa ni uzoefu mkubwa kwa Aaron," Giggs alisema, akizingatia dau kubwa la Bale wakati akijiunga na Real Madrid akitokea Tottenham mwaka 2013.

"Tazama kuhusu uwezeshaji wa Juventus walio nao, ni klabu kubwa.

"Anakwenda klabu kubwa, kubwa zaidi Italia.

"Anacheza vizuri kwa sasa na [na matarajio ya kuondoka Arsenal] hayawezi kumuathiri."

Giggs atakiongoza kikosi cha Wales katika mechi ya kirafiki dhidi ya Trinidad and Tobago Jumatano kuelekea mchezo wao wa kufuzu Euro 2020 dhidi ya Slovakia mwishoni mwa wiki.



## SOLSKJAER APANIA KUREJESHA MAKALI UTD

**MANCHESTER, England**

Ole Gunnar Solskjaer amewaahidi mashabiki wa Manchester United kwamba timu hiyo itarejea katiba ubora wake baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa, kufuatia kuonyesha kiwango kibovu zaidi tangu Mnorway huyo aanze kuiongoza.

United imekuwa katika wakati mgumu kufuatia kupoteza kwa mabao 2-1 ugenini dhidi ya Wolves kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la FA Jumamosi, na Solskjaer - ambaye amerithi mikoba ya Jose Mourinho Desemba mwaka jana - akihaha kwa kipigo cha pili mfululizo kwa mara ya kwanza katika uongozi wake.

'Mashetani Wekundu' hao walichapwa mabao 2-0 na Arsenal katika mechi yao muhimu ya Ligi Kuu, ikiwarejesha katika majanga baada ya kutoka kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Paris Saint-Germain kwenye mechi ya mkondo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora, matokeo ambayo yaliwafanya kusonga mbele hatua ya robo fainali kwa faida ya bao la ugenini.

Akizungumza na wanahabari kufuatia kiwango chao kibovu walichokionyesha katika Uwanja wa Molineux, Solskjaer aliulizwa endapo ana ujumbe kwa mashabiki wa United.

"[Tutakuwa tayari] kurejea tena baada ya mapumziko ya kimataifa," alisema.

"Man United Aprili na Mei mara zote inarejea katika kiwango chake, hatuwezi kusubiri kwa changamoto hii na usiku mkubwa wakati Barcelona itakapokuja, tuna mambo muhimu sana ya kutarajia," aliongeza akizingatia mechi dhidi ya miamba ya Catalunya kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Wachezaji? Usiwe na hofu kuhusu mtazamo wao kwa sababu wakati watakaporejea watakuwa vizuri tena tutawapa namna ya kuweza kuendela."

Mabao kutoka kwa Raul Jimenez na Diogo Jota katika nafasi ya sekunde sita na nusu yaliiweka Wolves katika umiliki, wakati bao la Marcus Rashford katika muda wa majeruhi likiwa limechelewa kwa United kuweza kutokea nyuma na kushinda, kiwango ambacho Solskjaer alisema kilikuwa kibovu zaidi tangu atue hapo.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA AMUONYA AGUERO KULAZA MIGUU

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amemtaka Sergio Aguero kuendeleza makali yake wakati wa mapumziko ya mechi za kimataifa.

Aguero alitokea benchi na kuivusha timu yake nusu fainali ya Kombe la FA kwenye mchezo wa robo fainali dhidi ya Swansea City, hilo likiwa ni bao lake la 28 msimu huu wakati wakitokea nyuma kwa mabao 2-0 na kushinda 3-2.

Straika huyo pia alimtengenezea Bernardo Silva bao la kwanza la City, wakati la kusawazisha likipatikana kutokana na mkwaju wake wa penalti kugonga mwamba na kujaa kimyani baada ya kipa Kristoffer Nordfeldt kuusindikiza kwa mguu.

Licha ya kiwango chake cha juu, Aguero, 30, kwa mara nyingine hakujumuishwa katika kikosi cha Argentina kuelekea mechi mbili za kirafiki dhidi ya Venezuela na Morocco.

Hiyo ikiwa inamaana atapata mapumziko kabla ya kurejea City kuendelea kuipigania klabu hiyo kutwaa makombe, lakini Guardiola hataki kuona nyota huyo akipumzisha sana miguu yake.

"Amemtaka, 'tafadhali jifue kidogo wiki hii, usipoteze utimamu wako kimwili' kwa sababu sasa yupo katika kiwango cha kushangaza," aliwaambia wanahabari baada ya mechi dhidi ya Swansea.

"Ninapenda [mchezo huu] kwa sababu tumecheza katika namna tofauti na washambuliaji wawili. Ni vizuri kuishi katika hali hiyo kwa sababu mara nyingine, kwenye baadhi ya mechi, tutahitaji hilo - kuweka watu wengi ndani ya boksi.

"Sergio ni wa kipekee. Kwa sasa yupo katika kipindi ambacho washambuliaji wakubwa pekee wanacho."

Kuwa fiti kwa Aguero kutaongeza nafasi ya kutwaa Kombe la EFL na City kuongeza nafasi ya kubeba mataji manne. Kabla ya mechi za jana ilikuwa pointi moja mbele ya Liverpool kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu, na pia wapo robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo watavaana na Tottenham huku pia wakiwa kwenye nusu fainali ya Kombe la FA.

Lakini kwa mara nyingine Guardiola hataki kabisa kukaribisha mazungumzo hayo huku akisisitiza kujipanga zaidi kwa wachezaji wake.

"Ninawasikiliza watu, wachezaji wa zamani, ambao wanasema kama hushindi Ligi ya Mabingwa Ulaya itakuwa ni kushindwa kwa hali ya juu, kama utashinda tu Kombe la Ligi utakuwa ni msimu mbovu," alisema.

"Sielewi wakati wao ni wachezaji wa zamani [wanaojua] ni kwa namna gani ilivyo vigumu kutwaa Kombe la Ligi ilivyo vigumu kutwaa Ligi ya Mabingwa, ni vipi wanaweza kusema mambo ya namna hii kwa klabu yetu. Sisi ni wapya katika aina hii ya nafasi.

"Sisi ni Manchester City, tunapaswa kutwaa Ligi ya Mabingwa? Unaongea kuhusu nini?

"Kilicho muhimu kwa klabu hii ni kuwapo pale, hivyo kwa vizazi vijavyo - makocha wapya na wachezaji wapya - watatambua kizazi kimoja cha wachezaji kilipigana kwa kila mchezo, katika kila shindano hadi mwisho.

"Huo ndio ubora tunaweza kuwa nao. Hicho ndicho cha muhimu kuliko kutwaa kombe. Ndicho walichotumia Manchester United wakiwa na Sir Alex Ferguson, Barcelona, Real Madrid, Bayern Munich, Juventus - aina hizi za timu kila msimu walikuwapo pale.

"Kwetu sisi, hiyo ni habari kubwa. Baada ya pointi 100 msimu uliopita, msimu huu katika hatua hii na makombe mawili mfukoni [ikiwamo Ngao ya Jamii] tupo pale, tukipambana kila mechi. Huo ndio ubora tunaoweza kuonyesha."

## KWA UFUPI

**MADRID KUMRUDIA DE GEA**

Real Madrid inataka kumsajili kipa wa Manchester United, Mhispania David de Gea, 28, kufuatia Zinedine Zidane kurejea katika klabu hiyo. ***(Sunday Mirror)***

**ARSENAL KWA WAN-BISSAKA**

Arsenal ipo tayari kumsajili beki wa kulia wa Crystal Palace, Aaron, licha klabu yake kuhitaji pauni milioni 40. ***(Sun on Sunday)***

**ICARDI, PERISIC SOKONI**

Inter Milan ipo tayari kumuuza straika Muargentina, Mauro Icardi, 26, na Mcroatia Ivan Perisic, 30, wakati huu Manchester United na Arsenal zote zikivutiwa na huduma ya wachezaji hao. ***(La Gazzetta Dello Sporto - in Italian)***

**COURTOIS NJIA PANDA REAL**

Zinedine Zidane amesema hakuna uamuzi wa mwisho uliokwisha kufanywa kuhusu mustakabali wa baadaye wa kipa Mbelgiji Thibaut Courtois katika klabu hiyo. Kipa huyo mwenye umri wa miaka 26 ambaye alisajiliwa baada ya Zidane kuondoka Mei 2018, alisugulishwa benchi katika mechi ya kwanza ya kocha huyo raia wa Ufaransa tangu arejee. ***(Evening Standard)***

**BUFFON, ALVES HAKIELEWEKI PSG**

Paris Saint-Germain imesimamisha mazungumzo ya mkataba mpya na kipa Muitaliano Gianluigi Buffon, 41, beki wa kulia Mbrazil Dani Alves, 35, na beki Thiago Silva, 34, baada ya miamba hiyo ya Ufaransa kutolewa kwenye kinyang'anyiro cha Ligi ya Mabingwa Ulaya na Manchester United. ***(L'Equipe - in French)***

**ERIKSEN KUITOBOA MADRID**

REAL Madrid ipo tayari kumsajili kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen, lakini klabu hiyo ya Ligi Kuu England inahitaji pauni milioni 200 kwa Mdenmark huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Sunday Star)***

**GUARDIOLA AMTETA SANCHO**

KOCHA Pep Guardiola amesema winga wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, 18, "hataki changamoto" kwa kujaribu kuwa katika kikosi cha kwanza Manchester City. Sancho aliachana na klabu hiyo ya Ligi Kuu England Agosti 2017. ***(Sky Sports)***

**BALE CHAMBO YA HAZARD**

Real Madrid inaweza kumuuza straika raia wa Wales, Gareth Bale, 29, kwa Chelsea kama sehemu ya kubadilishana na kiungo Mbelgiji Eden Hazard, 28. ***(Sunday Express)***

**SESSEGNON AWINDWA SPURS**

Tottenham inaandaa ofa ya pauni milioni 50 kwa winga wa Fulham, Ryan Sessegnon, 18, ambaye pia ameivutia Manchester United na Paris Saint-Germain - wakati huu akiwa bado hajasaini mkataba mpya na Fulham. ***(Sunday Mirror)***

**POCHETTINO AMFUATA FILIPE**

Mauricio Pochettino ametuma mashushu kwenda kumtazama straika wa Benfica, Mreno Joao Pedro Neves Filipe, 19. ***(Sunday Star)***

**DR CONGO KUMSHAWISHI WAN-BISSAKA**

DR Congo inataka kumshawishi beki wa Crystal Palace, Aaron Wan-Bissaka kuichezea timu hiyo ya taifa. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 alizaliwa jijini London na ana asili ya Congo. ***(Independent)***

**SILVA AMSHUKIA MINA EVERTON**

KOCHA wa Everton, Marco Silva, amemwambia beki Mcoolombi, Yerry Mina, 24, anahitaji kuwa thabiti kama anataka kupata nafasi mara kwa mara katika kikosi cha kwanza. ***(Sky Sports)***

HABARI MICHEZO

# CHAMA AGAWA ZAWADI KWA MASHABIKI SIMBA

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO wa Simba, Clatous Chama, amesema bao la ushindi alilofunga juzi kwenye mchezo wa mwisho wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita, amelitoa kwa mashabiki wa timu hiyo ambao wamekuwa wakiwasapoti.

Chama juzi alifunga bao hilo muhimu na kuifanya Simba kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 na hivyo kufuzu hatua ya robo fainali.

Chama alisema mashabiki wa Simba wamekuwa wakiwasapoti muda wote, hivyo na wao kama wachezaji wamekuwa wakipambana uwanjani ili wasiwaangushe.

"Na bao la ushindi ambalo nimefanikiwa kufunga ni maalum kwa mashabiki wa Simba na shukrani kwa kuendelea kutusapoti," alisema Chama.

Alisema kwa sasa wanaangalia mbele zaidi baada ya kufuzu hatua hiyo ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Bao hilo la Chama lililowapa ushindi Simba alilifunga dakika ya 88 akikumbushia bao la ushindi kwenye mchezo wa mtoano kuwania kuingia hatua ya makundi dhidi ya Nkana ya Zambia ambayo Simba ilishinda mabao 3-1 shukrani kwa bao la dakika za mwisho la Chama.

Simba sasa inasubiri Jumatano kumjua mpinzani wake kwenye hatua ya robo fainali wakati droo itakapochezeshwa jijini Cairo, Misri.



Ofisa Michezo wa Manispaa ya Ubungo, Fredrick Kadewele (wa tatu kulia), akimkabidhi cheti mmoja wa washiriki wa kozi ya awali ya soka, Ahmed Prezidaa, katika hafla iliyofanyika juzi, jijini Dar es Salaam. **PICHA: SOMOE NG' ITU.**

## Wahitimu kozi ya ukocha wapewa neno

**Na Mwandishi Wetu**

OFISA Michezo wa Manispaa ya Ubungo jijini Dar es Salaam, Frederick Kadewele, amewataka wahitimu wapya wa kozi ya awali ya mpira wa miguu kwenda kutumia kwa vitendo mafunzo waliyopata ili kusaidia kuinua maendeleo ya soka Tanzania.

Kadewele alisema hayo juzi wakati akikabidhi vyeti kwa wahitimu 27 wa kozi hiyo iliyoandaliwa na Chama cha Soka Wilaya ya Ubungo (UFA) na kuendeshwa na Mkufunzi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Kiongozi huyo alisema endapo makocha hao hawatayatumia mafunzo waliyopata kwa kufundisha timu mbalimbali kuanzia za vijana, watakuwa hawajaitendea haki elimu hiyo waliyoipata.

Alisema kozi kwa ajili ya makocha wa timu za michezo mbalimbali zitaendelea kuandaliwa katika manispaa hiyo kwa sababu malengo ya Ubungo ni kuona kila timu inakuwa na mwalimu ambaye ana taaluma inayotambuliwa rasmi.

"Napenda kuwaambia UFA kuwa ofisi yangu itaendelea kushirikiana nanyi ili kuhakikisha tunakuwa mfano hapa nchini, tunataka kuona timu zote zinakuwa na walimu wenye taaluma, nawakumbusha kuwa mnatakiwa kutoka kitaaluma kutoka kiutendaji, usipotoka kiutendaji hautakuwa na maana," alisema Kidewele.

Kiongozi huyo alisema pia manispaa yake itamlipia ada ya kozi ya ngazi ya kati mshiriki, Fadhila Kizigo, ambaye alikuwa mwanafunzi pekee mwanamke kati ya washiriki 27 waliokabidhiwa vyeti pamoja na wengine watatu waliopata alama A katika kozi hiyo iliyomalizika.

Naye Katibu Mkuu wa UFA, Frank Mchaki, aliishukuru TFF na Chama cha Soka Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA) kwa kushirikiana nao kufanikisha kozi hiyo na kwamba wanaahidi kuendelea kuendesha mafunzo mengine zaidi katika manispaa hiyo.

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.YANGA | 28 | 21 | 4 | 3 | 45 | 19 | 67 |
| 2.AZAM | 28 | 17 | 8 | 3 | 46 | 18 | 59 |
| 3.SIMBA | 20 | 16 | 3 | 1 | 43 | 7 | 51 |
| 4.LIPULI | 31 | 11 | 11 | 9 | 26 | 26 | 44 |
| 5.KINONDONI MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 6.MTIBWA SUGAR | 29 | 12 | 5 | 12 | 30 | 23 | 41 |
| 7.TZ PRISONS | 30 | 9 | 11 | 10 | 24 | 25 | 38 |
| 8.COASTAL UNION | 30 | 8 | 14 | 8 | 27 | 30 | 38 |
| 9.MBEYA CITY | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 10.ALLIANCE | 30 | 9 | 10 | 11 | 23 | 30 | 37 |
| 11.MWADUI | 31 | 10 | 6 | 15 | 35 | 39 | 36 |
| 12.KAGERA SUGAR | 29 | 8 | 12 | 9 | 23 | 27 | 36 |
| 13.JKT TANZANIA | 31 | 8 | 12 | 11 | 18 | 26 | 36 |
| 14.MBAO | 30 | 9 | 9 | 12 | 19 | 29 | 36 |
| 15.STAND UTD | 31 | 10 | 6 | 15 | 29 | 40 | 36 |
| 16.RUVU SHOOTING | 30 | 8 | 11 | 11 | 27 | 35 | 35 |
| 17.SINGIDA UTD | 30 | 8 | 9 | 13 | 20 | 31 | 33 |
| 18.NDANDA | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 19.BIASHARA UTD | 29 | 7 | 9 | 13 | 21 | 29 | 30 |
| 20.AFRICAN LYON | 31 | 4 | 10 | 17 | 19 | 39 | 22 |

# Ufaransa kuleta sanaa ya msosi

**Na Beatrice Shayo**

UBALOZI wa Ufaransa hapa nchini umeandaa sanaa ya kutayarisha vyakula vya kiutamaduni wao kama sehemu ya kutunza mazingira.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam na Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, wakati akizungumza na waandishi wa habari, ambapo alifafanua kuwa nchi yake ina lengo la kushirikiana na Tanzania katika masuala mbalimbali ikiwamo pamoja na utamaduni.

Alisema tukio hilo litafanyika Machi 21, mwaka huu, ambapo watakuwa wanasherehekea na kutambua tamaduni zao kwa Tanzania.

Clavier alisema nchi hiyo imeongeza pia misaada yake zaidi ya mara mbili iliyotolewa mwaka uliopita na kwamba inapenda kuona Tanzania pia inafikia malengo yake ya kuwa nchi ya viwanda mwaka 2025.

Balozi Clavier alisema siku hiyo inayotambulika kama 'Gastronomy Day' kutakuwa na vyakula vya aina mbalimbali ambavyo vitaandaliwa hapa nchini na wapishi wataalamu kutoka Ufaransa, vinywaji kama mvinyo na shampeni pamoja na burudani pia kutoka Ufaransa.

**Balozi huyo aliipongeza Tanzania kwa jitihada zake za kudumisha tamaduni zake hapa nchini na hasa katika upande wa vyakula jambo ambalo ni mfano nzuri.**

Alisema anafurahi kuishi Tanzania na angependa atakapostaafu arudi kuwekeza katika sekta hiyo ya utamaduni husussan kwenye vyakula.

Aidha, Clavier alisema nchi yake inaungana na mapambano dhidi ya uharibifu wa mazingira ya baharini unaotokana na matumizi mabaya ya plastiki. Kwa upande wake Meneja Mkuu wa Hoteli ya Hyatt, Garry Friend, alisema kuwa wanatarajia kupokea mpishi mkuu kutoka Ufaransa, Francois Lucchesi ambaye atashirikiana na wapishi wengine wa hoteli hiyo kuandaa chakula hicho.

"Tunashukuru sana kwa heshima ambayo Tanzania na hoteli yetu imepewa na ubalozi wa Ufaransa kuandaa chakula hiki, tunawaalika watu wote kuja kushiriki tukio hili la kihistoria," alisema.

Alisema tukio hilo la kitamaduni litajenga uwezo wa wapishi wa hapa nchini katika kuandaa chakula cha nchini Ufaransa pamoja na kujifunza mambo mengine ya nchi hiyo.

Michezo
Jumatatu Machi 18, 2019
Nipashe



## Guardiola amuonya Aguero kulaza miguu

HABARI UK 30

KITU HICHO...



Gareth Bale akiifungia Real Madrid bao la pili, wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Celta Vigo kwenye mechi ya kwanza ya La Liga kwa Zinedine Zidane kuiongoza timu hiyo, tangu aliporejea kwa mara nyingine kuinoa. Bao la kwanza lilifungwa na Isco. **HABARI UK. 28**

# SIMBA MDOMONI MWA ESPERANCE

## Nafuu kwake ni kwa Mamelodi, TP Mazembe, Aussems atoa sababu za ushindi huku...

**Na Mwandishi Wetu**

KUJITUMA na kufuata maelekezo ndio moja ya sababu iliyoelezwa na Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, kufuatia ushindi wao wa mabao 2-1 kwenye mchezo wao wa mwisho wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita, ambapo sasa ipo katika nafasi ya kukutana na Mamelodi Sundowns, Esperance ama TP Mazembe.

Simba juzi iliibuka na ushindi huo, hivyo kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika, shukrani kwa mabao ya Mohammed Hussein 'Tshabalala' na Clatous Chama.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mchezo huo, Aussems alisema wapinzani wao walicheza soka zuri, lakini amewasifu wachezaji wake kwa kujituma na kufuata maelekezo yake kikamilifu.

"Lazima niwapongeze wachezaji wangu... wamefanya kile nilichowaelekeza..., tulihitaji ushindi kuweza kufuzu hatua ya robo fainali, wapinzani wetu walikuwa bora, lakini nafikiri sisi tulikuwa bora zaidi yao," alisema Aussems.

Alisema kila mmoja aliyepata nafasi ya kucheza juzi alipambana kwa ajili ya timu.

"Na hata mabadiliko niliyoyafanya yalikuwa ya kiufundi, lengo lilikuwa kushambulia zaidi baada ya kuwa tupo nyuma kwa bao moja," alisema Aussems.

Kwa ushindi huo wa juzi, Simba inakuwa timu ya kwanza kutoka Tanzania kufuzu hatua ya robo fainali tangu michuano hiyo ianze kuendeshwa kwa mfumo mpya mwaka 1997 na inaungana na All Ahly kufuzu hatua hiyo kutoka Kundi D lililokuwa likijumuisha pia JS Saoura iliyomaliza nafasi ya tatu.

**Robo Fainali**

Simba ambayo imemaliza nafasi ya pili ikiwa na pointi tisa nyuma ya Al Ahly yenye alama 10, sasa inasubiri droo itakayochezeshwa Jumatano Cairo, Misri kujua mpinzani wake ajaye.

Kwa mujibu wa Kanuni za Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF) linalosimamia michuano hiyo, Simba itakutana na moja ya timu iliyoongoza makundi mengine matatu na si kutoka katika kundi lake, Al Ahly.

Kwa mantiki hiyo Simba inaweza kukutana na kinara wa Kundi A, Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini ama bingwa mtetezi aliyeongoza Kundi B, Esperance ya Tunisia au kuangukia kwa TP Mazembe ya DR Congo kutoka Kundi C.

Timu zinazoweza kukutana na Al Ahly ni zilizoshika nafasi ya pili katika makundi mengine ambazo ni Wydad Casablanca ya Morocco kutoka Kundi A au Horoya ya Guinea kutoka Kundi B ama Constantine ya Algeria iliyokuwa Kundi C.

Hatua ya robo fainali mechi hizo zitaanza kuchezwa kati ya Aprili 6 na 7, huku mechi za marudiano zikitarajiwa kupigwa Aprili 13 na 14, mwaka huu.

# Yanga yalilia bahati Iringa

**Na Mwandidhi Wetu, IRINGA**

LICHA ya kipigo cha bao 1-0 walichokipata kutoka kwa Lipuli ya Iringa, kocha msaidizi wa Yanga, Noel Mwandila, amesema timu yake ilicheza vizuri, lakini walikosa bahati kwenye mchezo huo.

Mwandila, alisema walitengeneza nafasi nyingi za kufunga, lakini hawakuwa makini kwenye kuzitumia.

**"Wenzetu wamepata nafasi wameitumia... sisi tulikuwa na nafasi nyingi kuweza kushinda lakini hatukuzitumia, kwangu naona tulikosa bahati kuweza kupata ushindi," alisema Mwandila ambaye aliachiwa jukumu la kukiongoza kikosi hicho kutoka kwa Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera aliyesafiri kwenda kwenye majukumu ya timu ya Taifa ya DR Congo.**

Aidha, alisema kupoteza mchezo huo wa juzi hakujawakatisha tamaa ya kuendelea kufanya vizuri kwenye ligi.

"Bado tuna michezo mingine mbele yetu, tuna mchezo mmoja wa Kombe la FA, tunaenda kujipanga kuweza kufanya vizuri kwenye michezo hiyo ya mbele yetu," alisema Mwandila.

Kipigo hicho cha juzi kinaifanya Yanga sasa kupoteza mechi tatu msimu huu, lakini inaendelea kuongoza ligi ikiwa na pointi 67 ikifuatiwa na Azam FC yenye pointi 59, huku timu zote zikiwa zimecheza mechi 28. Simba ambayo imecheza michezo 20 inashika nafasi ya tatu ikiwa na alama 51.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >